**Jengo** la jipya DDC kubadili sura Kariakoo

UKURASA 3


**Wananchi** walia kero maegesho ya malori

UKURASA 8



**Israel** yaonya hali Ukanda wa Gaza si shwari

UKURASA 17




UKURASA 9


# Nipashe Jumapili

Jumapili Januari 7, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0589024

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Rungu LATRA latua Kilimanjaro Express

**KWA** kupandisha nauli holela, mabasi ya wanafunzi kufuata... *Endelea ukurasa. 2*



Mabasi ya kampuni ya Kilimanjaro Express yanayofanya safari kati ya Dar es Salaam, Moshi na Arusha yamefungiwa kwa kukiuka masharti ya leseni. Picha ndogo kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Saluo. **PICHA: MAKTABA**

UKURASA WA 4

## DAKTARI AELEZA UONDOAJI UVIMBE BILA UPASUAJI

DAKTARI wa Hospitali ya Kairuki ya Mikocheni, Dar es Salaam, Fredy Rutachunzibwa, ameelezea teknolojia mpya duniani inavyotumika kutoa matibabu ya kuondoa uvimbe mwilini bila kulazimika kufanya upasuaji.

Mtambo unaotumika kuondoa uvimbe bila upasuaji unaoitwa 'High...

UKURASA WA 23

## TAIFA STARS KUTESTI MITAMBO LEO MISRI

TIMU ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' leo inacheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Taifa ya Misri ikiwa ni mchezo wa kujipima na kutesti mitambo yake kuelekea kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) yatakayoanza Januari 13 nchini Ivory Coast.

Mpaka kufikia leo wachezaji wote wameripoti kambini ambapo jana kundi...

# Uthubutu Samia mabadiliko sheria uchaguzi waikuna EU

UKURASA 4

## Biteko ataka Watanzania kuyalinda Mapinduzi

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YASHUSHA KIUNGO MKABAJI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Biteko ataka Watanzania kulinda, kuenzi Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ametoa wito kwa wananchi kuendelea kuyaenzi, kuyalinda na kuyaishi kwa dhamira ya dhati, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Amesema waasisi wa nchi walifanya mapinduzi hayo ili kuwa na taifa huru ambalo kila mtu anakuwa na hadhi, kuondoa dhuluma iliyokuwapo na kufanya wananchi kuishi kwa amani na furaha.

Akizungumza na wananchi jana katika Wilaya ya Mkoani, mkoani Kusini Pemba, baada ya kuzindua ofisi ya uhamiaji na makazi ya askari wilayani humo, alisema wananchi wanawajibu wa kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa kuyaishi.

Pia alisema wanatakiwa kuyaheshimu, kukuza uchumi wa nchi na kukuza uzalendo ili baada ya muda mrefu hata baada ya miaka 100 mbele, watakaokuja kuyasherehekea wakute Zanzibar iliyobora zaidi na waseme yaliwafaa.

"Moja ya tunu tulizo nayo ni mshikamano, hivyo watu wasiruhusu mtu yeyote kuwagawanya kwa misingi yoyote ile, bali maendeleo yaunganishe watu wote na tofauti za vyama, dini na kabila visifanye watu wakae kwenye makundi bali kuunganisha watu kwa maslahi ya nchi na Watanzania," alisema.

Dk. Biteko alisema nchi inapokwenda kusherehekea Siku ya Mapinduzi ya Zanzibar Januari 12, mwaka huu, Watanzania waungane kuwaombea Rais wa Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ili waendelee kuongoza vyema, kuimarisha ustawi wa taifa na kuwaunganisha watu.

Kuhusu jengo alilozindua, Dk. Biteko alisema kuwa ni moja ya matunda ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, kwani kabla ya hapo, watu walinyimwa haki zao za kimsingi zikiwamo za uhamiaji kama vile kupatapasi ya kusafiria.

Alisema mapinduzi yamewezesha wananchi kupata uhuru wa kusafiri nje ya mipaka ya nchi.

"Ofisi hii ya uhamiaji Wilaya ya Mkoani ilianza mwaka 1979 ikiwa ni ndogo, lakini sasa kuna jengo la kisasa litakalowezesha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi wa wilaya hiyo na viunga vyake, ikiwa ni kielelezo cha mafanikio ya Mapinduzi ya Zanzibar," alisema.

Dk. Biteko alipongeza viongozi wakuu wa nchi kwa juhudi wanazochukua ili wananchi wapate huduma bora ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Pia aliwapongeza viongozi wa idara ya uhamiaji kwa usimamizi wa jengo hilo na kuiagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuona namna ya kujenga jengo kama hilo katika wilaya mbalimbali nchini.

Alisema jengo hilo ambalo ni la kisasa limezingatia watu wenye mahitaji maalum na limechukua eneo dogo na kumejengwa kwa gharama nafuu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alimshukuru Rais Samia kwa mambo mema anayoyafanya kwa vyombo vya usalama ikiwamo kutoa vibali vya ajira, upandishaji vyeo, mafunzo, ulipaji madeni na kuwezesha vyombo vya usalama kwa kununua vitendea kazi.

Sigini alisema kuwa, idara ya uhamiaji imeendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na idara hiyo, ambapo mwaka wa fedha 2022/23, walilenga kukusanya Sh. bilioni 56.5 lakini wakakusanya Sh. bilioni 67.679.

Alisema katika mwaka huu wa fedha unaoendelea imekusudia kukusanya Sh. bilioni 75, lakini hadi mwezi Desemba ilikusanya Sh. bilioni 43.119 ambayo ni zaidi ya nusu ya malengo, huku matarajio ni kufikia malengo yaliyowekwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Islam Seif, alisema kuwa, ofisi ya uhamiaji ilianza kujengwa mwezi Agosti, mwaka 2022, na kukamilika mwezi Novemba, mwaka jana.

Alisema jengo hilo la kisasa litakidhi mahitaji ya sasa ikiwamo ya mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ambayo ni muhimu katika ufanyaji kazi. Gharama za ujenzi wa ofisi hizo ni Sh. bilioni 1.53.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alimshukuru Dk. Samia na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi na pia, kuboresha huduma mbalimbali za wananchi.

Alisema mafanikio mbalimbali yanayotokea sasa ni kutokana na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika mwaka 1964 ambapo pia, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliasisiwa na kuzaa taifa la Tanzania.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji (katikati), akiwa na Mkurugenzi wa Kampuni za MM Integrated Steel Mills Ltd (MMI), Ratish Kamania (kulia), na Mkurugenzi Mtendaji, Veer Patel, wakati wa ziara ya alipotembelea upande wa kiwanda cha kutengeneza rangi kati ya viwanda vitano, Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rungu LATRA latua Kilimanjaro Express

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imeyasimamisha magari yote ya Kampuni ya Kilimanjaro Express kutoa huduma ya usafirishaji kuanzia kesho kutokana na kukiuka masharti ya leseni ikiwamo kutotoa tiketi za kielektroniki na kuzidisha nauli kwa abiria.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam, baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika stendi ya mabasi ya Magufuli pamoja na ofisi za mabasi ya kampuni, zilizoko Ubungo Shekilango, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Suluo alisema mabasi hayo pekee ndiyo bado yanatoa tiketi zisizo za kielektroniki na kwamba yamebainika kukiuka masharti mengi ya leseni licha ya kuonywa mara kwa mara na kutozwa faini.

"Na leo (jana) tumelikamata gari lingine la kampuni hii ya Kilimanjaro inayofanya safari zake kati ya Dar es Salaam, Moshi na Arusha likiwa limezidisha nauli kwa abiria. Kila abiria alilipishwa nauli tofauti, tukawataka wawarejeshee nauli zao, wakakubali, lakini muda mfupi tumetoka kwenye ofisi zao, wakakataa kurejesha eti mpaka bosi wao aseme.

"Na hii si mara moja. Wamekuwa wakifanya hivi mara nyingi na tumewaonya mara kwa mara na wanaona kulipa faini ni kawaida kwao. Sasa sisi lengo letu ni kutaka wafuate sheria na masharti ya leseni, watoe huduma bora na si kutoa faini.

"Kama anaona kulipa faini ni kawaida kwake sisi hatuwezi kuvumilia, tumetoa maagizo asitoe huduma kuanzia Jumatatu mpaka atakapofanya maboresho na kufuata masharti ya leseni yake," alisema.

Suluo alisema mbali na kuwaonya, pia wamekuwa wakifanya nao vikao vya kuwasisitiza kufuata na kuheshimu masharti ya leseni yao lakini wamekuwa wakipuuzia.

"Sasa hii ni dharau kubwa ambayo hatuwezi kuendelea kuivumilia, lazima tuchukue hatua," alisisitiza Suluo.

Baadhi ya abiria waliokuwamo kwenye gari hiyo walisema walilazimika kulipa nauli hiyo kutokana na uharaka wa kusafiri.

"Najua nauli ya kwenda Arusha ni Sh. 42,000 lakini wamenitoza Sh.50,000 na nilikubali kutoa kwa sababu nilikuwa na haraka lakini awali niliwauliza wakaniambia nauli ndiyo hiyo licha ya kuwabishia na nilipopanda gari nikagundua kila abiria alikuwa ameambiwa nauli tofauti," alisema Erica Urio.

Mmoja wa Maofisa wa Kampuni ya Mabasi ya Kilimanjaro ambaye hakutaka kujitambulisha jina lake, alipoulizwa kuhusu sababu za kuzidisha nauli kwa abiria hao, hakutaka kujibu chochote.

**MABASI YA WANAFUNZI**

Akizungumzia mabasi yanayotoa huduma kwa wanafunzi, Suluo alisema kuanzia Jumatatu (kesho) wataanza kufanya ukaguzi wa leseni ikiwamo kuangalia hali ya magari yanayotumika kutoa huduma hiyo kama yana viwango kama masharti ya leseni yanavyowataka.

"Sisi ndio tunatoa leseni kwa mabasi hayo ya wanafunzi na ili tutoe leseni hizo lazima tupite kwenye shule kukagua na kujiridhisha na ubora wa magari yenyewe kama yana sifa za kutoa huduma kwa wanafunzi.

"Na hata kama tutabaini kwamba kuna shule zinatumia magari ambayo hayajakaguliwa na kupewa leseni tutachukua hatua," alisema.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ramadhani Ng'anzi, alifanya ukaguzi kwa magari ya wanafunzi katika wilaya ya Kinondoni.

Alisema katika kuelekea kufungua shule, jeshi hilo litafanya ukaguzi kwa mabasi yanayotoa huduma ili kuhakikisha magari hayo ni yale yaliyokidhi vigezo kwa usalama wa wanafunzi.

Huu ni mwendelezo wa LATRA kuchukua hatua dhidi ya wafanyabiashara katika sekta ya usafirishaji wanaokiuka miongozo, sheria na taratibu.

Desemba 10, 2023, LATRA ilifanya msako na kukamata mabasi 37 yanayotoa huduma ya usafirishaji mikoani kwa kosa la kuwazidishia nauli abiria na kutotumia tiketi za kielektroniki.

## HABARI KITAIFA

# Jengo jipya DDC kubadilisha sura Kariakoo

**Na Romana Mallya**

JENGO la Shirika la Uchumi la Jiji la Dar es Salaam (DDC) lililoko Kariakoo, linatarajiwa kuvunjwa mwishoni mwa mwezi huu ili kupisha uwekezaji mkubwa wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Jengo hilo ambalo kwa sasa linawafanyabiashara 130, baada ya uwekezaji huo kukamilika wafanyabiashara wanatarajiwa kuwa zaidi ya 400 na linatarajiwa kubadili mandhari ya Kariakoo.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, alisema kwa sasa jengo hili lina wafanyabiashara si chini ya 130.

"Mwishoni mwa mwezi Januari tunategemea wafanyabiashara wote wa eneo lile wawe wamehamia maeneo mengine kama tulivyokwisha kuelezana miezi saba iliyopita.

"Ifikapo Januari 31, 2024, tunatarajia kuanza kupachakata kwa ajili ya maandalizi ya awali ya uwekezaji huo," alisema.

Chalamila alisema uwekezaji huo utahusisha ujenzi mkubwa wa ghorofa kubwa ambalo ndani kutakuwa na maduka, kumbi, kituo kidogo cha polisi na huduma zinginezo nyingi zitakazotoa ajira kwa watu wengi.

Mkuu wa Mkoa alimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kwa kuona na kuridhia uwekezaji huo kufanyika.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, anasisitiza uwekezaji unaoalika sekta binafsi kuwa sehemu ya uwekezaji na serikali.

"Nani atakayeshughulikia, kwa kushirikiana na serikali tutajulishana kadri siku zinavyokwenda. Nitoe wito kwa wafanyabiashara wote wa eneo hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, atapita pia kutoa hamasa na elimu, ili wafanyabiashara waridhie mpango huu kama walivyoridhia awali.

"Kusiwe na vurugu za aina yoyote tunapoelekea kwenye uwekezaji huu mkubwa ambao utakuwa na tija zaidi kuliko sasa," alisema.

Mkurugenzi wa DDC, Ali Milambo, alisema ubomoaji huo utahusisha majengo yenye kumbi mbili na sehemu ya mbele ambako kuna ghorofa lenye benki.

"Eneo likishavunjwa lote kutajengwa jengo kubwa lenye maduka zaidi ya 400, ndani yake kutakuwa na kumbi za mikutano, benki hoteli, na kituo cha polisi kama ambavyo Mkuu wa Mkoa alivyosema.

Milambo alisema wanategemea uwekezaji huo utabadilisha mandhari ya Kariakoo hasa kwa kuzingatia lipo barabarani likizungukwa na mitaa ya Narung'ombe, Congo, Msimbazi na Muhonda.

"Kimsingi Karikaoo ni soko la kimataifa kwa hiyo maduka yatakayokuwa pale yatakuwa na mvuto mkubwa na kuongeza ajira kwa wananchi. Kwa sasa eneo kwa namna lilivyopangwa limechukua wafanyabiashara 130 tu.

"Baada ya uwekezaji kukamilika kutakuwa na maduka zaidi ya 400 na wafanyabiashara ndani ya jengo hilo wakiwa na angalau kila mmoja na watumishi watatu, hapo tunaongelea ajira kubwa kwa wananchi," alisisitiza.

DDC ni shirika la umma lililoanzishwa na serikali Mei, 18, 1971 chini ya sheria ya kampuni namba 212 ya mwaka 1971 mpaka 1973 lililopowekwa chini ya sheria namba 16 ya mashirika ya maendeleo ya Wilaya (District Development Cooperation Act no 16).

DDC lilianzishwa kama kitega uchumi cha Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam kwa lengo la kufanya shughuli za uzalishaji, biashara na burudani kwa ajili ya wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam.

Dira ya Shirika la DDC ni kuwa taasisi inayoongoza kiuchumi ndani ya ushindani kwa kutoa huduma yenye tija na za kudumu ndani ya jiji hilo.

## Hoja 5 Muungano zapatiwa ufumbuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jaffo, amesema wakati Zanzibar inaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Hussein Ali Mwinyi na Rais Samia Suluhu Hassan, hoja tano ambazo ni kero za muungano zimetatuliwa.

Amesema kulikuwa na hoja 25 za muungano, lakini mwaka 2010 hoja mbili zilipatiwa ufumbuzi na mwaka 2020 hoja tano zimepatiwa ufumbuzi, hivyo mpaka sasa zilizotatuliwa ni hoja saba.

Jaffo aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi ujenzi wa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano ya Kiwengwa Tembo Hotel inayojengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja, ikimilikiwa na mwekezaji mzalendo, Hussein Muzamill.

"Lakini kwa mapenzi na utashi wa kisiasa wa Rais Samia na Dk. Mwinyi tunaona mpaka leo ikiwa ni awamu ya kwanza (ya uongozi wao) wameondoa hoja 11 za muungano na kisha wakaondoa hoja nne takribani ndani ya kipindi chao, hivyo kuondoa changamoto za Muungano zipatazo tano,"alisisitiza.

Aidha, alisema katika kusherehehekea miaka 60 ya mapinduzi, kazi kubwa inaonekana hasa katika sekta ya afya, miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege ambayo itasaidia uwekezaji kwa kuwa, watalii wanapofika nchini huhitaji kusafiri kwa urahisi.

Jaffo alisema fedha za UVIKO-19 zaidi ya Dola za Marekani milioni 100 zimetumika vizuri Visiwani Zanzibar kubadilisha uchumi wake na kujenga hospitali nzuri kila wilaya, miradi ya maji safi na salama pamoja na shule nzuri za ghorofa.

"Muda si mrefu watu wataitembelea Zanzibar kushuhudia mapinduzi ya kiuchumi na kimaendeleo hasa katika upande wa uchumi wa buluu ambapo kuna uwekezaji wa hoteli katika sekta ya utalii," alisema.

Kuhusu mazingira, Jaffo aliwataka wawekezaji wanaowekeza katika miradi ya sekta ya utalii kuhakikisha wanalinda mazingira na kuepuka uharibifu wa fukwe za bahari.

Jaffo alisema miradi ya hoteli kwa kiasi kikubwa inahitaji kuwapo kwa mikakati ya kulinda mazingira ikiwamo fukwe kwa kuona hakuna uharibifu utakaotishia maisha ya binadamu na viumbe vya baharini.



Baiskeli zikiwa zimepangwa kwenye njia ya watembea kwa miguu huku watumiaji wa njia hiyo wakipita kwa tabu katika eneo la Karume Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Watatu waliogundulika na kipindupindu waruhusiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU watatu kati ya watano waliobainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa kipindupindu katika kata ya Kagongo Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wameruhusiwa baada ya afya zao kuimarika.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri hiyo, Dk. Shani Josephat, alisema jana kuwa wawili waliogundulika na ugonjwa huo wanaendelea na matibabu katika Kituo cha Afya Mwendakulima.

Dk. Josephat alisema Januari 2, mwaka huu, kuliripotiwa watu watano kuwa na dalili za ugonjwa wa kipindupindu hali iliyowafanya kuchukua sampuli zao na kuzipima katika maabara hospitalini hapo, huku zaidi ya 500 wakiendelea kuwa karantini.

"Tunaendelea na kukabiliana na tatizo hili kwa kuzitembelea kaya na kuzipatia elimu ya namna ya kujikinga kwa kufanya usafi wa mazingira yanayowazunguka, kwani ugonjwa huu ni hatari na unaua," alisema.

Alisema watu wanaobainika kuwa na ugonjwa huo wanapatiwa huduma katika Kituo cha Afya Mwendakulima na tayari wameelekeza nguvu katika kata hiyo ili kudhibiti ugonjwa huo usisambae.

"Timu yetu ya watalaamu wa afya imeweka kambi katika kata hiyo kwa ajili ya kutoa elimu ya namna ya kuzuia ugonjwa huo usiendelee kuenea zaidi kwenye kata nyingine.

"Mpaka sasa visa vyote vya ugonjwa huu viko ndani ya kata hii pekee na wale wanakaya walioruhusiwa tunawafuatilia kwa ukaribu ili wasije kupata ugonjwa huo kwa mara nyingine,"alisema Dk. Josephat.

Alisema wahisiwa wote waliopokelewa katika kituo hicho cha afya hakuna hata mmoja aliyepoteza maisha, wametibiwa na wengine wameruhusiwa.

Alisema mpaka sasa katika kituo cha tiba na mafunzo kuna wagonjwa 13 ambao pia, afya zao zinaendelea kuimarika.

Mkazi wa Kagongwa, Kevin Godgrey, alishauri kuzifikia kata nyingine na kuzipatia elimu ya kujikinga na ugonjwa huo, kwani baadhi yao wamekuwa wakifika katika kata hiyo kupata mahitaji ya familia.

# Uthubutu Samia mabadiliko sheria uchaguzi waikuna EU

Na Mwandishi Wetu



Rais Samia Suluhu Hassan.



Getrude Mongela.



Miapetra Kumpula -NATRI.



Susan Dossi.

WADAU wa kimataifa, ikiwamo Umoja wa Ulaya (EU), wamesifu utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika kuleta mabadiliko ya miswada ya sheria za uchaguzi kuwa utaimarisha demokrasia na ushiriki zaidi wa wanawake katika nafasi za uongozi.

Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2023 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Wakizungumza jana katika mjadala wa kitaifa wa miswada hiyo uliofanyika kwa njia ya mtandao, Mbunge wa Bunge la EU kutoka Finland, Miapetra Kumpula, alibainisha uzoefu wa Finland na EU katika kuongeza uwakilishi wa wanawake na vijana katika siasa.

Kumpula alisema hatua ya Rais Samia katika kuhakikisha kunakuwa na ushirikishwaji wa wanawake kwenye siasa na utawala, inachochea usawa wa kijinsia.

"Kama Umoja wa Ulaya umekuwa na uchaguzi wa wabunge kila baada ya miaka mitano na Finland ndiyo inaongoza kwa kuwa na wanawake katika siasa kwenye nchi ambazo ni wanachama wa EU.

"Tumekuwa na mifumo tofauti ya upatikanaji wa wanawake na wanaume kwa kuchaguliwa katika siasa," alibainisha.

Kuhusu uzoefu wakati alipokuwapo Rais wa kwanza mwanamke kwa Finland, alisema uwapo wake ulifungua milango ya kushiriki kwenye uongozi kwa wanawake na wasichana.

Alisema kuwa na kiongozi mwanamke kunaamsha wanawake na wasichana kuona kila mlango umefunguliwa kwa ajili yake na kushiriki.

"Rais Samia anafanya jitihada kubwa za kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uongozi. Anapaswa kuungwa mkono na watu wote katika kuleta usawa," alisema.

Mbunge wa Malawi na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Vyombo vya Habari na Mawasiliano, Susan Dossi, alisema katika Bunge la Malawi kuna wanawake 14 kati ya 193 ambao hujadili na kuweka mikakati ya namna ya kuongeza ushiriki wao.

"Nampongeza Rais Samia anavyofanya kwa Tanzania kuwawezesha wanawake kwenye nafasi za uongozi, nilisoma sehemu anavyoteua mawaziri kwa mfano, Waziri wa Ulinzi kuwa mwanamke.

"Hii ni kubwa na amekuwa akitengeneza mazingira mazuri kuleta mabadiliko ya namna hii, utashi wake wa kisiasa kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uchaguzi ni jambo linalohamasisha,"alisema.

Dossi alisema Rais Samia amekuwa akifanya jitihada za kuhakikisha wanawake wengi wanakuwa kwenye nafasi za uongozi.

"Alikuja Malawi akatembelea jamii na amekuwa mfano wa kuigwa kwa sisi wanasiasa wachanga wanawake wa Malawi. Ninafurahishwa na uongozi wake kuzingatia haki za binadamu na kuchochea demokrasia nchini kwake, kuvipa uhuru vyombo vya habari kupata habari,"alisema.

Pia alisema anafahamu wabunge wanawake wanapata nafasi ya ubunge wa viti maalum kupitia kuchaguliwa ndani ya vyama vyao, lakini ni vyema kwenda majimboni ili kuwa na mamlaka zaidi.

"Ninaomba kuhimiza kuhakikisha kuna mazingira jumuishi ya wanawake kushiriki kwenye uchaguzi za msingi kwa kuwa, wengi wanaoshiriki na kushinda ni wanaume. Ni wakati wa kuweka sheria nzuri za kufanya wanawake washiriki ipasavyo na kuchaguliwa badala ya kuwekwa na vyama vyao kwenye Bunge,"alisema.

Kuhusu viti maalumu, alisema si vibaya lakini wanawake wanashauriwa wagombee kwenye majimbo ili wachaguliwe kwa kupigiwa kura kwenye uchaguzi ili kuwa na wanawake wengi kwenye uongozi wanaochaguliwa na wananchi.

Alishauri kutungwa sheria inayolinda wanawake kwenye kampeni ili kutumika lugha za staha na si za kuwadhalilisha kwa kuwa wengi wanaogopa kushiriki kwenye uchaguzi kutokana na kudhalilishwa.

Seneta Catherine Mumma kutoka Kenya, alisema wabunge wanawake wa Kenya na Afrika wanajivunia uongozi wa Rais Samia na amekuwa mfano mkubwa wa kuigwa kwao.

"Rais Samia ameonyesha uongozi unaozingatia haki za binadamu, uhuru kwa vyombo vya habari, haki ya kukusanyika na kutoa nafasi kwa wadau wa siasa kutoa maoni yao," alisema.

Alisema ni mwanadiplomasia bora na wanajivunia uongozi wake Rais Samia kwa kuwa, kama taasisi ya kusaidia wanawake wengine kujifunza kwenye uongozi.

"Hii inadhihirisha sasa wanawake watapewa nafasi kubwa kwenye uongozi si tu Tanzania na nchi zingine kutokana na utendaji kazi wake alioonyesha wanawake wanaweza," alisema.

Kadhalika, alisema kuwapo na miswada ya mabadiliko ya sheria za uchaguzi zinazochochea demokrasia nchini ni utashi wa kisiasa wa Rais Samia.

"Kenya tumeweka vyema suala la usawa wa kijinsia tumeweka hivi kwamba nafasi za kuchaguliwa lazima ziwe na theluthi mbili ya wanawake.

"Ni muhimu kuwa na mikakati ambayo italeta usawa ili huko mbeleni tusijikute tena tuna wanawake wengi kushinda wanaume,"alisema.

Alisema katika miswada ya sheria inayotolewa maoni na wadau nchini Tanzania ni muhimu kuweka asilimia fulani ya wanawake katika kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye nafasi za uongozi.

Mwanasiasa Mkongwe, Getrude Mongela, alisema usawa wa jinsia si jambo la kuomba na mabadiliko ya sheria yatawafanya wanawake kuwa na uhuru katika kuchangia maendeleo ya nchi.

"Ni vyema katika miswada hii kuangalia bila kuondoa rushwa kwenye uchaguzi mwanamke kila siku hatapata nafasi, sisi tulipitia mfumo wa kuombaomba.

"Ninaomba na mimi mniweke, hakukuwa na rushwa ya ngono, sisi tulikuwa tunaomba kusimama na kujieleza,"alisema.

Mongela alisema mwanamke asipewe nafasi kwa kuangalia jinsia yake, bali achaguliwe kwa hoja kwa kuwa, wana karama ya uongozi.

**MAONI YAPOKEWA**

Katika hatua nyingine, Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imeanza kupokea maoni ya wadau kuhusu miswada hiyo.

Mmoja wa wadau ni Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ambaye aliwasilisha rasmi mapendekezo ya chama chake ikiwamo Tume ya Uchaguzi kusimamia chaguzi zote, ikiwamo wa serikali za mitaa na kuomba kamati kuliangalia suala hilo.

Zitto ameshauri uchaguzi wa mwaka huu usimamiwe kwa mpito na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

## HABARI KITAIFA

# Daktari aeleza uondoaji uvimbe bila upasuaji

**Na Mwandishi Wetu**

DAKTARI wa Hospitali ya Kairuki ya Mikocheni, Dar es Salaam, Fredy Rutachunzibwa, ameelezea teknolojia mpya duniani inavyotumika kutoa matibabu ya kuondoa uvimbe mwilini bila kulazimika kufanya upasuaji.

Mtambo unaotumika kuondoa uvimbe bila upasuaji unaoitwa 'High Intensity Focused Ultrasound (HIFU), tayari umeshaanza kufanya kazi kwenye hospitali hiyo kuanzia mwezi huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dk. Rutachunzibwa ambaye alipata mafunzo hayo nchini China, alisema mtambo huo tiba unatibu uvimbe wa aina mbalimbali kwa kutumia mwangwi wa ultra sound.

Teknolojia hiyo, alisema ni ngeni kwenye nchi nyingi za Afrika na haitumiii mionzi kama ambavyo imezoeleka kwenye tiba nchini, hasa zinazohusiana na masuala ya uvimbe.

"Huu mtambo tiba unatibu uvimbe mbalimbali na hautumii mionzi. Kinachofanyika ni kwamba yale mawimbi sauti yanabadilishwa kwenda kwenye mfumo wa nishati joto (heat energy) na yanakwenda kuchoma sehemu yenye uvimbe tu bila kuathiri maeneo ya jirani yanayozunguka uvimbe huo.

"Mfano kama uvimbe uko kwenye kizazi ina maana mayai hayatahusika kwenye tiba hiyo. Ni uvimbe tu ambao utachomwa bila kuathiri maeneo ya jirani na kama ni kwenye titi tu basi kutachomwa kwenye uvimbe lakini sehemu zingine hazitaathirika kinachoathirika ni uvimbe tu," alisema

"Tukishauchoma uvimbe tuna uwezo wa kuangalia hapo hapo je tumefanikiwa kwa kiasi gani? Kama kutaonekana bado kuna kitu cha kurudia, tutarudia lakini baada ya muda mfupi uvimbe unaanza kupungua na utapungua hadi utaisha kabisa na mhusika ataendelea na maisha yake kama kawaida," alisema.

Pia alisema kwa mgonjwa ambaye amefanyiwa tiba hiyo wanatarajia ndani ya siku nne au tano uvimbe utaaanza kuisha taratibu kwasababu baada ya kuuchoma mwili unakuwa na kazi ya kuvunja vunja vile vilivyokuwa kwenye uvimbe na kuviondoa nje ya mwili kama takataka.

Alisema wanapomaliza tiba wanaendelea kumfuatilia mgonjwa kila baada ya miezi mitatu ili kuangalia mwenendo wa kupungua na hatimaye kumalizika kabisa kwa uvimbe.

Maandalizi ya kumwingiza mgonjwa kwenye mtambo huo kwa ajili ya kuanza matibabu hayo, alisema ni pamoja na kumtaka mhusika asile chakula chochote ndani ya saa nane kabla ya kuingizwa kwenye mtambo.

Alisema mgonjwa anapofika kutaka kuondolewa uvimbe, anapimwa upya kwa vipimo vya Ultra Sound, MRI na CT Scan vya hospitalini hapo ili kujiridhisha na aina ya uvimbe wanaotaka kuutibu.

"Lazima tuangalie kwanza tunatibu uvimbe wa aina gani, je ni uvimbe unaosambaa au uvimbe ambao hausambai, kama ni ule ambao hausambai lazima mtaaalamu achukue sehemu ya nyama akapime tuthibitishe kama ni uvimbe ambao hausambai," alisema

"Hata kama tukibaini uvimbe huo unasambaa unatibika kulingana na hatua aliyofikia mgonjwa, mfano ikionekana mhusika ana saratani ya ziwa lazima tujue uvimbe huo umeshasambaa au bado na ikitokea haujasambaa inawezekana kuutibu na ukaondoka kabisa," alisema.

Alisema faida za tiba kwa kutumia mtambo huo ni kwamba mgonjwa hapati maumivu makali, anapata nafuu haraka, hapotezi damu na anaepukana na makovu ya upasuaji.

Alisema mtambo huo ni wa nne kwa Afrika na kwamba uko pia kwenye nchi za Misri, Afrika Kusini, Nigeria na sasa uko Tanzania kwenye hospitali hiyo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akisisitiza jambo kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati) alipokwenda kukagua eneo watakalohamishiwa waathirika wa mafuriko yaliyotokana na maporomoko ya mawe na tope kutoka mlima Hanang juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Rose Kamili. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Waziri Pinda akagua eneo jipya waathirika wa mafuriko Hanang

**Na Munir Shemweta,** KATESH

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ametembelea na kukagua eneo ambalo limepimwa viwanja kwa ajili ya kuwahamishia waathirika wa mafuriko yaliyotokana na maporomoko ya mawe na tope kutoka Mlima Hanang mkoani Manyara.

Pinda alifanya ukaguzi huo juzi akiambatana na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, na viongozi wengine wa mkoa na wa wilaya ya Hanang.

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeshiriki pamoja na wadau wengine katika kutathmini kiwango cha uharibifu uliotokana na maafa yaliyotokea Desemba 3, mwaka jana, na kushauri juu ya maeneo yanayoweza kutumika kuhamishia waathirika.

Akiwa katika eneo hilo, Pinda alielezwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Manyara, Wenceslaus Mtui, kuwa ekari 100 kutoka Jeshi la Magereza kwenye eneo la Warret, zimetolewa kwa ajili ya waathirika hao.

Desemba 21, mwaka jana, Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jeniste Mhagama, alielekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhakikisha viwanja kwa ajili ya kuwahamishia waarhirika maeneo ya Gendavi, Jorodom, Ganana na Katesh - Hanang vinapimwa na kukamilika kabla ya Desemba 31.

Kwa mujibu wa Mtui, upimaji viwanja katika eneo hilo lililotolewa na Jeshi la Magereza umefanyika kwa weledi na kukamilika ndani ya siku saba na kwamba viwanja 269 vilipimwa na kupandwa mawe.

Alisema viwanja vilivyopimwa viko katika mgawanyo wa makazi 226, makazi na biashara 26, na huduma za jamii 17. Hata hivyo, alisema suala la uandaaji hati linasubiri maelekezo pamoja na orodha rasmi iliyohakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, aliishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kufanya kazi kubwa ya kupima viwanja na kuweka mawe katika muda mfupi.

" Nikushukuru wewe pamoja na wizara yako na utufikishie salamu kwa Waziri wa Ardhi kwa kufanya kazi ndani ya muda mfupi na si tu kupima bali na kuweka mawe," alisema Sendiga.

Naibu Waziri Pinda alisema wizara yake imeshafanya jukumu lake la msingi la kupima eneo hilo na kutoa wito kwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuharakisha uchongaji barabara kuelekea eneo hilo ili kurahisisha usafirishaji vifaa.

"Nimwombe Mkurugenzi Mkuu wa TARURA na kupitia wizara yake waone umuhimu wa kuharakisha barabara zifike hadi site (eneo la viwanja), alisema Pinda.

## Waziri abainisha dhamira serikali

**Na Lusajo Mwakabuku,** NJOMBE

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Pindi Chana, amesema serikali imedhamiria kuhakikisha mradi wa chuma na makaa ya mawe wa Liganga na Mchuchuma unatekelezwa mapema.

Amesema hatua hiyo ni kutokana na serikali kuwalipa fidia wananchi wote waliopisha eneo la utekelezaji wa mradi huo mkubwa ulioko Ludewa mkoani Njombe.

Waziri Chana alisema hayo juzi akiwa katika Kijiji cha Nkomang'ombe, Ludewa akiwa katika ziara ya siku mbili akitekeleza jukumu la kusimamia misingi iliyowekwa na Sheria Sura 449 na 450 yenye lengo la kuhakikisha uwekezaji katika uvunaji na matumizi ya utajiri asili na maliasilia za nchi unatekelezwa kwa namna ambayo inainua hali ya wananchi kiuchumi na kuongeza pato la taifa.

"Lengo la ziara hii ni kufuatilia utekelezaji wa sheria hizi katika miradi ya Liganga na Mchuchuma. Sheria hizi zinaweka misingi ya kuhakikisha wananchi wa Ludewa na walioko karibu na maeneo ya miradi wananufaika na fursa zinazopatikana katika uwekezaji wa rasilimali za taifa.

Kwa mfano, ni matarajio ya serikali kuwa uwekezaji wa namna hii utatoa ajira kwa Watanzania, utatoa fursa ya Watanzania kusambaza zabuni na kuwapa mafunzo yanayolenga kuhuisha teknolojia kwani kwa kufanya hivyo ndiyo utekelezaji wa misingi iliyowekwa na sheria zetu," alisema.

Aidha Waziri Chana alisema pamoja na kwamba mradi huo una historia ndefu, Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha nia ya wazi ya kutekeleza kwa kutoa fedha ili uanze kazi mara moja baada ya maafikiano ya kimkataba kufikiwa.

Waziri Chana pia alizungumza na wananchi wa vijiji vya Nkomang'ombe na Mundindi ambavyo miradi hiyo inatekelezwa na kuwataka wawaandae vijana wao katika nyanja mbalimbali zikiwamo elimu, uwekezaji mdogo mdogo na ujuzi ili mradi utapoanza, waitumie nafasi hiyo kuwa wanufaika wa kwanza wanakuwa wananchi wa maeneo husika.

Mmoja wa wanufaika wa fidia kutokana na mradi huo, Raphael Memba, mkazi wa kijiji cha Nkomangombe, alimshukuru Rais Samia kwa kutimiza ahadi yake ya kulipa fidia licha ya kusubiri muda mrefu.

Pia aliomba serikali kuhakikisha taratibu mbalimbali zinazokwamisha mradi huo kuanza, zinapatiwa ufumbuzi haraka ili ulete mafanikio kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali inastahili kongole kwa kusitisha vifurushi vipya NHIF

**HIVI** karibuni, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulitangaza vifurushi vipya vya matibabu kwa wanachama wake ambavyo vilipangwa kutumika kuanzia Januari Mosi, mwaka huu, katika vituo vya kutolea huduma za afya zikiwamo hospitali za serikali na zile za binafsi.

Kwa mujibu wa taarifa ya NHIF, vifurushi hivyo vipya vilionyesha mabadiliko ya ada ya usajili na ushauri wa daktari viwango ambavyo vilionekana kushuka kulinganisha na vile vya awali.

Gharama za kumwona daktari kwa mfano, kwa Hospitali ya Taifa vilishushwa kutoka Sh. 35,000 hadi Sh. 25,000 kwa daktari bingwa mbobezi na Sh. 25,000 hadi Sh. 20,000 kwa daktari bingwa. Kwa hospitali za rufani za kanda, kumwona daktari bingwa mbobezi viwango vilipunguzwa kutoka Sh. 35,000 hadi Sh. 25,000 na kumwona daktari bingwa kutoka Sh. 25,000 hadi kufikia 20,000.

Katika hospitali za rufani za mkoa, kumwona daktari bingwa mbobezi kiwango kilipanda hadi Sh. 25,000 kutoka Sh. 15,000 na kwa daktari bingwa ni Sh. 20,000 kutoka Sh. 15,000. Kwa upande wa kliniki bobezi, kumwona daktari bingwa mbobezi na daktari bingwa kiwango kimepungua kutoka Sh. 15,000 na kufikia Sh. 10,000, huku kwenye kliniki kumwona daktari bingwa na bingwa mbobezi ni Sh. 10,000.

Kutokana na kutangazwa kwa viwango hivyo, kuliibuka mvutano kati ya wamiliki wa hospitali binafsi na NHIF hali iliyotishia kuwapo kwa mgomo kwa wamiliki wa hospitali binafsi. Sababu kubwa iliyotolewa ni kutokushirikishwa kwa watoa huduma hao binafsi ambao kwa kiasi kikubwa, wana mchango wenye kutukuka katika sekta ya afya. Jambo hilo kwa mtazamo wa wamiliki hao, ni kwamba wanaburuzwa katika uamuzi unaofanywa kuhusu utoaji wa huduma za afya.

Hali hiyo imesababisha serikali kutangaza kusitishwa kwa matumizi ya vifurushi hivyo vipya. Pia taarifa iliyotolewa na NHIF juzi ilisema serikali pia imeunda kamati huru itakayofanya mapitio na kuwasilisha mapendekezo yake serikalini.

Kusitishwa kwa vifurushi hivyo, kumefanyika baada ya serikali kukutana Alhamisi wiki hii na watoa huduma kutoka sekta binafsi pamoja na NHIF kwa lengo la kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ya kitita cha mafao kinachotarajiwa kuanza kutumika kwa wanachama wake. Baada ya majadiliano, ndipo Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alipoagiza kuundwa kwa kamati huru kwa ajili ya kufanya mapitio na kuwasilisha mapendekezo serikalini kabla ya kuanza kutumika. Kamati hiyo imepewa muda mfupi kwa kufanya kazi hiyo na kuwasilisha taarifa ndani ya mwezi huu.


Kwa jumla, wazo la NHIF lilikuwa zuri kwa kuwa kama ilivyosema katika taarifa yake. Pamoja na kuwa na wazo zuri katika kufanya hivyo, ni dhahiri kwamba hivyo kutokana na mwenendo katika misingi yoyote ya utawala bora, suala la ushirikishaji wadau ni la muhimu.

Kwa mantiki hiyo, NHIF katika siku zijazo inapaswa kushirikisha wadau katika utoaji wa huduma za matibabu ili kusitokee mkanganyiko kama ulivyojitokeza baada ya kufanya mabadiliko hayo. Tanzania inaongozwa na misingi ya utawala bora ambayo katika moja ya nguzo zake ni ushirikishwaji wa wadau katika masuala ya uamuzi. Wadau ndio msingi mkubwa katika utoaji maoni ili serikali ipokee na kuboresha badala ya kujifungia na kuamua kwa matakwa yake na kuamuru wahusika wapokee na kutekeleza pasi na kupewa nafasi.

Serikali kwa upande wake, kutokana na hatua iliyochukua ya kusitisha matumizi ya vifurushi hivyo vipya, inastahili pongezi na imeonyesha wazi kwamba inatekeleza kwa matendo kauli yake kwamba inawajali wananchi wake. Ni dhahiri inawajali wananchi kwa kuwa vinginevyo kama vifurushi hivyo vingeachwa na kuanza kutumika, waathirika wakubwa wangekuwa wananchi ambao wangekosa huduma katika vituo vya kutolea matibabu vinavyomilikiwa na mashirika na watu binafsi. Ni Imani kwamba kamati huru iliyoundwa itafanya kazi zake kwa weledi na kuwasilisha mapendekezo serikalini kupitia wizarani kwa mchakato zaidi. Pia ni Imani kwamba mapendekezo yatakayotolewa yatazingatia maoni na mawazo ya wadau katika utoaji huduma za afya na kwa manufaa ya wananchi ambao ndio watumiaji wakubwa wa huduma hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Kamanda Ng'anzi, umeupiga mwingi

**MAKOSA** ya kibinadamu, uzembe wa baadhi ya madereva wa mabasi na magari binafsi, vinatajwa kuchangia kuwapo kwa ajali za barabarani zinazogharimu maisha ya watu na wengine na ulemavu wa kudumu.

Kutokana na mazingira hayo, Desemba Mosi, mwaka jana, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani lilifanya operesheni ya kuwakagua madereva na kufuta leseni na kuwashusha madaraja madereva 45.

Wengine miongoni mwa hao, wamefikishwa kortini wakituhumiwa kuvunja sheria za usalama barabarani, ambapo wanatokea mahabusu ya polisi kwenda kusikiliza kesi zao.

Hayo ni kwa mujibu wa Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi (SACP) Ramadhan Ng'anzi, wakati akielezea mafanikio ya operesheni hiyo, kwamba wakihitaji leseni, watatakiwa kurudi darasani tena waangaliwe kama wamekidhiki sifa za kupata madaraja.

Katika ufafanuzi wake Kamanda Ng'anzi, ni kwamba madereva 24 wamefungiwa kwa kuharibu na kuchezea mfumo wa kufuatilia mabasi (VTS), wengine 21 wakifikishwa mahakamani.

Aidha, anasema makosa ya kibinadamu, uzembe wa baadhi ya madereva, ni chanzo cha ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu, na kwamba kikosi chake kimeamua kukabiliana na uzembe huo.

SACP Ng'anzi anaweka wazi kuwa ndani ya hiyo Desemba madereva 1,095 walitozwa faini za papo hapo kwa kosa la kuendesha gari zaidi ya kilomita 90 kwa saa ambazo hawatakiwi kuzivuka.

Nimeeleza kwa kirefu mrejesho ambao Kamanda Ng'anzi ameuleta kwa Watanzania baada ya operesheni hiyo ya Desemba, lakini niseme kwamba ipo haja kwa madereva kubadilika na kutambua wajibu wao.

Kimsingi, madereva wa mabasi, wamebeba dhamana ya roho za abiria na wao wenyewe, hivyo, umakini wawapo barabarani ni jambo la muhimu, ili waweze kuwafikisha abiria wao kule wanakokwenda.

Ni kweli kwamba ajali haina kinga, lakini kwa sababu inaelezwa kuwa ajali nyingi zinazotokana na uzembe na ubinadamu, ninadhani bado madereva wanatakiwa kuchukua hatua za kuwa makini.

Inasikitisha kuona dereva akiendesha gari akiwa amelewa, huo ni uzembe ambao kwa kweli hauwezi kukubalika kwa mtu anayethamini uhai wa binadamu wenzake. hivyo operesheni iliofanywa na Kikosi cha Usalama Barabarani, iwasaidie madereva kupunguza ajali.

Madereva wanathamini maisha yao na ya maisha ya abiria wao walionao katika vyombo vyao vya moto. Watambue kuwa wamebeba roho nyingi za abiria wenye matumaini ya kufika salama kule waendako.

Ingawa ajali haina kinga, lakini ninaamini kuwa njia pekee ni kuzingatia sheria za usalama barabara hata wakati mwingine ajali ikitokea haiwezi kuwa madhara makubwa kama yale yanayosababishwa na uzembe.

Lakini pia abiria nao hawana nudi kuchukua hatua za kutoa taarifa kwa vyombo husika wanapoona dereva anafanya uzembe aidha kwa kuendesha basi kwa mwenda mkali ama awe ameelewa.

Abiria wakifanya sehemu yao kwa kuwaripoti katika mamlaka husika, ninaamini matokeo chanya yanaweza kupatikana katika mapambano dhidi ya ajali za barabarani zinazosababishwa na uzembe.

Kila upande ukifanya sehemu yake, madereva kuthamini maisha ya wengine, abiria kutoa taarifa, hakutakuwa na ajali za kizembe, badala yake watakoa maisha yao, abiria, wapita njia na watembea kwa miguu.

Nakumbuka kumewahi kuwapo na kampeni ya kutomeza ajali za barabarani iitwayo 'Dereva thamini maisha yako, ya abiria na wengine', ikilenga kuwajengea madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Waliacha wapi kaulimbiu hiyo? Ninadhani wanapaswa kurudi nyuma waikumbuke, kwani lengo lake lilikuwa ni kuwambusha waepuke ajali ambazo wana uwezo wa kuziepuka.

Ajali zinaacha majonzi kwa familia, ukoo, jamii na taifa na kuathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo. Hivyo ninaamini wale ambao wamekumbwa na operesheni na Desemba watakuwa wamejifunza kitu na kubadilika.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Siasa si ajira, ni kazi ya kujitolea



Pascal Mayalla

WIKI hii, nilihudhuria mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa kujadili miswada mitatu ya Sheria ya Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa, na Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Mkutano huo ulifanyika jijini Dar es Salaam, ulifunguliwa na Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na kufungwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko.

Nianze na pongezi, kwanza kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunda kikosi kazi kilichosababisha mabadiliko haya ya sheria hizi. Pili, kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kwa kutualika watu kama sisi ambao si viongozi wa vyama vya siasa, lakini ni wadau muhimu wa siasa za nchi yetu.

Kusema kweli nilichoshuhudia kwenye mkutano huu, kwenye masuala nyeti ya kisheria kama haya, vyama vyetu vya siasa ni kama hakuna kitu kabisa. Msaada mkubwa na michango mikubwa ya maboresho ya sheria hizo, umetoka kwa wadau ambao si vyama vya siasa, wakiwamo Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), kilichowakilishwa na mwanasheria na wakili msomi Alex Mgongolwa.

Pongezi zangu za tatu, ziende kwa vyama vya siasa na haswa kwa chama kikuu cha upinzania, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuhudhuria mkutano huu baada ya maridhiano na kukubaliana kugawana nusu mkate.

Baada ya maridhiano na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kukubaliana kugawana kiti kinachoitwa "Nusu Mkate", kwa sababu baada ya kuususia ule mkutano wa kwanza wa Dodoma, nikawaomba msisuse, niliandika Makala yenye kichwa Chadema, Tafadhali Msisusie Mkutano Wa Vyama, Wasilisheni Hoja Zenu Mezani, Zitamfikia Samia, Ana Nia Njema Na Nchi Hii, Mpeni Ushirikiano!.

Kususa kule kukawa na faida kwa CHADEMA, kukazaa matunda ya maridhiano, lakini kususia Mkutano wa pili uliofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam, hakukuwa na manufaa yoyote. Katika mkutano huu wa tatu, nikawatumia Chadema ombi mahusus "Nawaombeni sana, msiendelee kususa na kuzira, hata kama mna hoja, njooni mezani, zileteni mezani, tukae pamoja, tuzijadili pamoja, tukiwa wamoja, ili twende pamoja!. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, kuna vitu, ili ufanikiwe, vinahitaji nguvu ya pamoja. CHADEMA wakalipokea ombi hili, wakaja mezani.

Kwenye mikutano yote miwili, nilibahatika kupata fursa ya kuchangia maoni na mawazo yangu na siku zote nimekuwa nikichangia kuhusu lile ambalo kwangu naliona ndilo kubwa kuliko na muhimu kuliko hata sheria zenyewe. Ni hitaji la mabadiliko madogo ya katiba kwanza, ili kuondoa ubatili fulani kwenye katiba, unaonyima haki ya kuchagua na kuchaguliwa, kisha ndipo tuje kwenye sheria.

Hili la ubatili wa katiba, kwa vile ni la kisheria, masikini vyama havilioni. Tunakwenda kubadili sheria ya zamani yenye ubatili, na kwa sababu ubatili huo, uko kwenye katiba, na hakuna mabadiliko ya katiba, hivyo tunakwenda tena kutunga sheria nyingine mpya yenye ubatili. Sijui kwa nini hili la ubatili wa katiba wenzetu hawalioni!

Mchangiaji mmoja akapendekeza tutenge asilimia 10 ya bajeti ya taifa, ilipwe kama ruzuku kwa vyama vyote vya siasa nchini! Mimi katika mchango wangu, hili nililipinga nikasema: "Ndugu zangu wa vyama vya siasa, wenzetu nchi za Ulaya, uongozi wa chama cha siasa ni utumishi wa umma wa kujitolea, uongozi wa chama si ajira.

Niliendelea kusema: "Vyama vya siasa tangu TANU havikuwa vinapewa ruzuku, vilikuwa vinasaidiwa fedha na wapenzi na wanachama. Ifikie mahali tuingie huruma na imani Watanzania wengi ambao wanaishi kwenye lindi la umaskini uliotopea, kwa nini tuendelee kuvipa vyama vya siasa ruzuku kwa kuwalipa watu wazima bukheri wa afya, wenye viungo vyao timamu, tuwalipe kwa kupiga domo?"

Hili la kupinga ruzuku, sikuanza nalo leo. Enzi za Rais John Magufuli (Mungu amweke pema) niliandika: "Asiyefanya kazi na asile". Je, siasa nayo ni kazi ya kustahili ujira wa mshahara kwa jina la ruzuku kwa vyama vya siasa? Ruzuku hii iendelee kuwapo watu waendelee kuitafuna au ifutwe?

Japo sijafanya utafiti wa ni nchi ngapi zinagawa ruzuku kwa vyama vya siasa, kwa nchi masikini kama Tanzania, serikali inayowajibika kwa watu wake na kuheshimu rasilimali kiduchu za taifa, haiwezi fedha zinazokamuliwa kama kodi kwa wananchi masikini wa kutupwa wanaishi kwenye lindi la umasikini uliotopea, halafu zinakuja kugawiwa bure kama ruzuku kwa vyama vya siasa, watu wazima wenye nguvu zao, na viungo vyao timamu, wanalipwa wazitafune kwa kazi ya kupiga domo!

Katika kuunga mkono juhudi za Rais Magufuli za kubana matumizi ikiwamo kupunguza safari za nje, kuwaengua watumishi hewa, kufanya tumbuatumbua majipu ya ufisadi, nilimshauri aziangazie ruzuku kwa vyama vya siasa.

Enzi za Nyerere kulitolewa ruzuku ya mbolea, mbegu bora na pembejeo za kilimo ili kuimarisha uzalishaji mali. Sasa ruzuku hizo zimefutwa na badala yake mijitu mizima isiyo na matatizo yoyote au changamoto za kiafya, ndiyo inatafuna ruzuku ya bure bure huku masikini wakitaabika.

Asiyefanya kazi na asile! Siasa si kazi ya mshahara bali ni kazi ya kujitolea. Ruzuku kwa vyama vya siasa ni ufisadi, ifutwe?.

**Paskali**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mechi za CCM FC vs Upinzani FC mwaka huu, mwakani



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

SIASA za Tanzania ni kama mchezo wa soka ambao una timu mbili zinazopambana kumpata mshindi, huku zikifanyiana rafu na fitina za hapa na pale.

Katika soka hilo la kisiasa, kuna timu mbili za CCM FC na Upinzani FC ambazo zote zinawania kubeba kombe kila baada ya miaka mitano lakini CCM FC imekuwa bingwa wa siku zote, huku Upinzani FC ikiendelea kupambana.

CCM FC imejaaliwa wachezaji wengi wakiwamo wastaafu walioichezea tangu ikiwa inajulikana kama TANU FC ikiwa na tawi lake Zanzibar lililojulikana kama Afro Shirazi FC nayo ikinyanyasa visiwani.

Tunawakumbuka wachezaji kama Jukanye, Abaka, Ahamwi, Ajumwi, Bwimka, Idawa, Jamki, Jopoma, Abema, Amoshe, Saaju na wengineo waliopata kuchachafya Upinzani FC kwa miaka yote hiyo.

Mwaka 1977 klabu hizi ziliungana na kuwa na CCM FC ambayo inaendelea kunyanyasa katika Ligi ya Taifa na kuinyima raha kabisa Upinzani FC ambayo nayo ina wastaafu lakini wanaonekana kulala sana.

Kinachofanya CCM FC kunyanyasa kila miaka mitano, ni Upinzani FC kukosa mshikamano wa pamoja wa kupambana na jitu hilo kubwa lililoanza soka miaka mingi ikilinganishwa na Upinzani FC.

Zamani miaka ya 1960, kulikuwa na Upinzani FC ambayo hata hivyo haikuwa na nguvu kiasi cha kuuawa na kutoweka kabisa katika ulimwengu wa soka, mpaka iliporejea mwaka 1992 ikiwa na wachezaji kama Maama, Chremti, Chrikatu, Asafu na wengine.

Hata hivyo, baadaye wakasajiliwa wachezaji kama Alyam, Frambo, Zimwaka, Tuali, Ihali, Jaframba na wengine kutoka Bara huku Seshaa, Juduha na Shakham na wengine wakitoka visiwani kuimarisha timu ya Upinzani FC.

Lakini hawakukosekana wachezaji waliojifanya mchana kucheza Upinzani FC lakini usiku wakionekana kwenye mazoezi ya CCM FC na hivyo kupunguza nguvu ya Upinzani FC na kubaki ikilalamika kila mechi ya kombe kuwa marefa wamekuwa wakiiuma.

Hivyo makombe yote kwa miaka yote hiyo yamerundikana katika makao makuu ya klabu ya CCM FC pale Dodoma, huku Upinzani FC ikiendelea kung'ara macho ikiwa mikono mitupu na kushindwa kutumia udhaifu wa CCM FC.

Kama zilivyo timu za Simba na Yanga, mara moja moja timu hizi mbili za kisiasa za CCM FC na Upinzani FC zimekuwa zikichukuliana wachezaji huku mashabiki wakibaki kulalamika na kukosa la kufanya na kumwachia Mungu.

Hata hivyo, safari hii kuelekea nusu fainali mwaka huu na fainali mwakani, CCM FC inaonekana kujikwaa mahali kwa wachezaji ndani kwa ndani kusigana, na wengine kuondolewa na kocha wake na kuwekwa benchi na kuingizwa wengine.

Kosa kubwa lililofanywa na CCM FC ni kumrejesha mchezaji ambaye miaka ya nyuma alicheza rafu mbaya sana dhidi ya wachezaji wenzake kwenye timu yake na hata vwakati mwingine kupiga mateke mashabiki na washangiliaji.

Mchezaji huyo mkorofi, Pachma, alilalamikiwa sana na mashabiki wa soka nchini wakati huo akilindwa na kutetewa sana na kocha ambaye hivi sasa ametangulia mbele za haki, akawekwa pembeni na sasa mwalimu wa sasa anadhani atamsaidia, na kumrejesha.

Baada ya kumrejesha huku Upinzani FC ikihoji sasa itakuwaje kutokana na mcheza rafu mashuhuri kurejea, mshambuliaji mahiri wa CCM FC Dagocho, naye akaamua kutundika daluga na kukaa pembeni kuangalia timu inavyoendelea.

Haijulikani kama Dogocho aliacha kwa sababu ya Pachma kurejea kundini kuchezea timu, lakini kuna mambo yalizushwa dhidi yake akaona ni fitna ambazo hawezi kuzivumilia na kujiweka pembeni.

Hata hivyo, inaonekana Upinzani FC inashangilia kuwa CCM FC imepungua nguvu kutokana na kuingia kwa mcheza rafu na kuondoka kwa mashambuliaji ambaye walikuwa wakiamini angeweza kuipa ushindi CCM FC kiulaini.

Ukweli ni kuwa safari hii CCM FC itatarajiwa kucheza vizuri na kwa utulivu mkubwa, bila kutegemea kuotea kama ambavyo imekuwa ikifanya na kubebwa na waamuzi, kwa sababu sasa yawezekana VAR itakuwapo katika mechi zote tena kwenye viwanja vyote.

Kwa kipindi kifupi, CCM FC imesababisha watazamaji wake kuangalia mechi zake gizani tena bila kula kutokana na kushindwa kumudu kununua vyakula vilivyopanda bei.

CCM FC imekuwa ikisababisha ubaguzi miongoni mwa mashabiki na watazamaji huku wengine wakipewa nafasi ya kukaa maeneo mazuri huku pia wakisamehewa viingilio wakati wa Upinzani FC wakinyimwa haki zao kwa makusudi.

Tumeshuhudia wachezaji wa CCM FC wakifumbiwa macho pale wanapocheza rafu, huku wa Upinzani FC wakioneshwa kadi za njano na nyekundu kila walipogusana na wa CCM FC.

Bila shaka mechi za mwaka huu hazitakuwa kama za mwaka 2019 na za mwakani hazitakuwa kama za mwaka 2020, mshindi halali atapatikana.

**Inshallah!**

# DED ataka ufaulu wanafunzi asilimia 100

**Na Steven William,** MUHEZA

MAOFISA elimu wote na wakuu wa shule za msingi na sekondari wilayani Muheza, mkoani Tanga, wametakiwa kutumia mbinu mbalimbali kusimamia taaluma ili kuhakikisha ufaulu unaongezeka hadi kufikia asilimia 100 mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, aliyasema hayo juzi alipotembelea na kukagua ujenzi wa maabara Shule ya Sekondari Mkurumuzi, ujenzi wa vyoo vipya vya sekondari hiyo pamoja na madarasa ya Shule ya Msingi Muheza Estate.

Akiwa, katika ziara hiyo, Dk. Mhina amewaagiza maofisa elimu na wakuu wa shule zote kuja na mikakati ya kuboresha elimu kwa kupandisha ufaulu hadi asilimia 100 ya kitaifa.

Kiongozi huyo alisema hataki kusikia ufaulu wa asilimia 74 katika wilaya hiyo na kutaka kila mwalimu atimize majukumu yake na kufanya kazi kwa ushindani.

Dk. Mhina aliagiza wakuu wa shule kuweka utaratibu wa kufanya tathmini kila wiki kwa walimu na masomo wanayoyafundisha ili kubaini mapungufu na namna ya kutatua ili kusaidia kupima kutokana na matokeo. Alisema ni wakati sasa wa walimu na watendaji wengine, wakiwamo maofisa elimu kutoka fisini kwenda kwenye shule ambazo zina changamoto ili kuinua hali ya elimu kwa kufanya tathmini ya wanafunzi na kubaini kwa nini wanashindwa kuwa na matokeo mazuri.

"Twendeni tukafanye kazi, tuache ubosi. Twendeni tukafanye tathmini, tujue mwanafunzi gani? Anachangamoto ipi? Ili tuweze kuzikabili changamoto ambazo zinaturudisha nyuma kiwango cha elimu kwenye wilaya yetu.

"Kiongozi unaweka mikakati ili kuweza kupata matokeo mazuri ya ufaulu, tumia jitihada zako upate matokeo ili uweke alama," alisema Dk. Mhina.

Alisema viongozi wilayani hapa wanapaswa kufanya kazi kwa kujituma ili kuweka alama na kuwataka walimu wakuu kujituma na kujitoa zaidi kwenye kutoa elimu bora kwa wanafunzi kuongeza ufaulu.

Dk. Mhina alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda wananchi wilayani hapa ndiyo maana amepeleka fedha za miradi ya elimu takribani Sh. bilioni tatu ili kuboresha sekta hiyo.

Pia alisema Rais Samia amepeleka Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa la utawala la halmashauri katika eneo la Kijiji cha Lusanga.

Alisema ili kuhakikisha miradi inakwenda vizuri lazima fedha za serikali zisimamiwe vizuri pamoja na kujenga urafiki na wadau kuchangia fedha za kuendeleza ujenzi hata kusaidia vyoo vya shule.

Kiongozi huyo aliagiza kuhakikisha wanafunzi wote wanaingia kidato cha kwanza mwaka huu.

Alibainisha kuwa, wilaya hiyo kuna fursa nyingi zikiwamo uwekezaji wa viwanda pamoja na mradi wa bomba la mafuta.

Katika ziara hiyo pia, alitembelea kukagua soko la nafaka pamoja na soko la mboga mboga ambayo ukarabati wake unatarajia kuanza hivi karibuni.

Diwani wa Tanganyika, Shafii Chewaje, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi huyo kutembelea miradi kata hiyo, alisema kuwa kata yake inatekelezwa miradi ya ujenzi wa maabara ya sekondari Mkurumuzi, choo cha shule na ujenzi wa madarasa.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya KL International, Alphonce Mkama (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu Ukumbi wa Kingazi Resort, Nelson Mahenge, wakibadilishana mikataba jana ya kuweka kambi ya kuandaa shindano la wanawake la kukuza Kiswahili kwa nchi za Afrika, lijulikanalo kama Binti Afrika balozi wa Kiswahili litakalowekwa katika ukumbi huo uliopo Kijichi jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maegesho ya malori yawa kero makazi ya watu

**Na Thomas Wandiba, SAUT**

WAKAZI wa Mtaa wa Mkanyenye Kata ya Mbugani wilaya ya Nyamagana, jijini Mwanza, wameomba serikali kuingilia kati suala la malori kubadilisha barabara ya mtaa kuwa maegesho kwa muda mrefu ya magari yao.

Wamesema hali hiyo inahatarisha usalama wao na familia zao ikiwamo uchafuzi wa mazingira.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii, baadhi ya wananchi hao walisema kuhamishiwa kwa maegesho mtaani hapo ni hatari husussani pale wanapokuwa na dharura za wagonjwa au moto, vyombo vya dharura haviwezi kufika kutokana na barabara kuzibwa na malori hayo.

"Madereva na wasaidizi wao hawana maeneo maalum ya kujisaidia, hivyo kujisaidia ovyo katika mazingira yetu hali inayohatarisha afya zetu hususani katika kipindi hiki cha mvua. Magonjwa ya milipuko yanaweza kuibuka,"alisema Asha Julius, mkazi wa mtaa huo.

Asha alisema barabara za kutokea na kuingia katika eneo hilo zimezibwa na malori hayo na kusababisha huduma za bajaji na bodaboda kusitishwa katika mtaa huo kwa kukosa mahala pa kupita.

Kadhalika, alisema wafanyakazi wa malori hayo hutupa viazi vilivyoharibika katika maeneo hayo na kusababisha uchafuzi wa mazingira ikiwa ni pamoja na harufu mbaya iliyotapakaa mtaani hapo.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Malori Mkoa wa Mwanza, Mtunza Hazina wa chama hicho, Eva Nyange, aliomba madereva wote wa malori katika eneo hilo kuzingatia taratibu na kanuni za usafi wa mazingira kwa sababu uchafuzi wa mazingira haukubaliki hata wao inawaweka katika hatari ya kupata magonjwa.

"Tulielekezwa na serikali kuhamia hapa, tukitokea Mbugani Sokoni, hivyo hali ya hapa hata kwetu sisi siyo rafiki, kwani eneo ni dogo jambo linalosababisha msongamano wa magari, hivyo tunaomba serikali kuangalia upya namna ya kuboresha mazingira ya eneo hili yawe rafiki kwa shughuli zetu au kutupangia eneo lingine mahususi," alisema Nyange.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Dastan Kisaka, alipotafutwa na Nipashe, alikiri kuwapo kwa kero hiyo pamoja na kupokea mara kwa mara malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kuzibwa kwa barabara hiyo.

Kisaka alisema uamuzi wa kuweka maegesho eneo hilo yalifanywa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza ambao ndiyo wanahusika na masuala ya maegesho ikiwa ni pamoja na kutoza ushuru wa maegesho.

"Nitakaa na Mkurugenzi wa Jiji pamoja na uongozi wa nkoa ili tuone namna ya kutatua kero hii, kwani wao ndiyo wana wajibu wa kubaini maegesho na kuchukua tozo za maegesho husika, hivyo tukishafikia muafaka itakuwa suluhu ya tatizo hilo.

# Hospitali yaongeza mapato ya ndani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UWEKEZAJI mkubwa katika sekta ya afya unaofanywa na serikali umesaidia kuiongezea uwezo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kukusanya mapato ya ndani.

Kutokana na uwekezaji huo, hospitali hiyo katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2023/24 (Julai hadi Septemba 2023), imeingiza Sh. bilioni moja.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Daniel Nkungu, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Dk Nkungu alitolea mfano huduma ya CT-Scan pekee imechangia kuongezeka kwa mapato ya ndani na kuanzia Septemba 2022 ilipoanza kutumika hadi Septemba, mwaka jana, imehudumia takribani wagonjwa 1,000 kwa kulipia gharama ya kipimo ya Sh. 150,000.

Alisema kuongezeka kwa mapato hayo ya ndani kumetokana na malipo ya papo kwa papo ya uchangiaji na mapato yanayotokana na wateja wa bima ya afya.

"Mapato yetu mengi yanatokana na kulipia huduma mbalimbali na mapato yamepanda kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali na pia utolewaji wa huduma ya CT Scan" alisema Dk. Nkungu.

Alisema huduma mbalimbali zimeongezwa ikiwamo uboreshaji wa vyumba vya upasuaji eneo la Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), uboreshaji wa vipimo, maabara, vitanda na kuendelea kufanya mabadiliko ya vitanda vya kulalia wagonjwa

"Yako maboresho makubwa tumeyafanya na gharama ziko zile zile za zamani za kiwango cha chini ili kumwezesha mwananchi kuzimudu kulipa," alisema Dk. Nkungu.

Alisema wamenunua gari aina ya Toyota Landcruiser kupitia mapato ya ndani kwa kuweka kidogo kidogo tangu miaka mitatu iliyopita (2021), hivyo kulipa kwa Wakala wa Serikali Sh. milioni 120 baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Mpango huu ulianzishwa na Mganga Mfawidhi aliyekuwapo wakati huo, Dk. Rita Lyamuya, ambaye matokeo hayo ni juhudi zake ya kuhakikisha ya kwamba Hospitali ya Rufani ya Mkoa inakuwa na magari," alisema Dk Nkungu.

Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, aliipongeza hospitali hiyo kwa kununua gari kwa ajili ya matumizi ya kiutawala kutokana na fedha mapato yake ya ndani.

"Kwa awamu tatu sasa ubunge wangu ninapokuja katika hospitali hii sijawahi kusikia mapato ya ndani yamenunua gari, lakini sasa mmefanya. Ninawapongeza sana," alisema Abood.

# MAISHA

Januari 7. 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*





# NI AIBU KUVAA KIGODORO?

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA









| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| K | ■ | N | D | E | G | E |
| U | ■ | ■ | ■ | L | ■ | N |
| N | ■ | M | K | E | ■ | D |
| G | I | A | ■ | Z | E | E |
| U | ■ | M | B | A | ■ | S |
| R | ■ | B | ■ | ■ | ■ | H |
| U | T | O | R | O | ■ | A |


## AMSHA AKILI


JAZA MAJINA YA MATUNDA UYAONAYO KATIKA VISANDUKU VILIVYOWAZI.













## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

NAO, TII, ZNZ, MTI, IGIZO, TINGA, IBANE, NDIZI, IGIZANA, SHIMONI

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA

Alichokifanya Adaktari



MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kulima bustani ya mboga pembeni ya nyumba yao. Wakati wanalima Juma alianza kumuuliza mama yake.

Juma: Eti mama ni kweli mchuma janga hula na wakwao?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima watakula pamoja

Juma: Kwani janga ni tunda hadi ale na ndugu zake?

Mama: Mwanangu huo ni msemo unaomaanisha kila baya unalolitafuta, utaathirika pamoja na ndugu zako, hivyo ni lazima kujiepusha.

**SWALI**

Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mwanamke kumtesa mtoto wa mwanamke mwenzie ni aibu

KARIBU tena msomaji. Leo nizungumzie unyanyasaji wa watoto unaofanywa na wazazi/walezi. Tunajadili ujumbe mfupi wa msomaji wetu kuhusu manyanyaso anayoshuhudia dhidi ya mtoto aliye jirani naye.

Ujumbe unasema: "Kwa jina naitwa Jerry (siyo jina halisi), naishi Mwanza wilaya ya Ilemela, kata ya Nyakato, Buzuruga. Kuna dada mmoja ameolewa na baba mmoja. Huyu dada ana watoto wawili wa kike.

Lakini pia baba huyu anaye mtoto mmoja wa kiume aliyemzaa nje. Baba akitoka mama humnyanyasa huyo mtoto wa kiume bila sababu. Dada anasahau mtoto wa mwenzio ni wako", anamaliza ujumbe wake.

Mama Salma Kikwete, mke wa Rais Awamu ya Nne, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Jakaya Kikwete kwenye mikutano inayohusu malezi ya mtoto wa kitanzania aliwahi kusema;

Anasema: "Tunaposema mtoto wa mwenzio ni mwanao tunamaanisha; sote tunapaswa kuwajibika kwa ajili ya ulinzi na ubora wa maisha ya watoto toka wakiwa tumboni hadi kuzaliwa na kusimamia maadili na makuzi yao.

"Watanzania wenzangu, tuache kulaumiana juu ya maadili ya vijana wetu, turejee malezi ya wazee wetu ili kila mmoja awajibike kumuona mtoto wa mwenzake kuwa ni wa kwake na kumrekebisha pale anapokosea. Usibague mtoto wako na wa mwenzio kwani wote ni watoto na wanakutegemea kwa ulinzi kamili katika kila jambo".

Tumemsikia mama huyo toka kwenye ujumbe wa Jerry hapo juu jinsi anavyomyanyasa mtoto ambaye mumewe alimzaa nje.

Pengine mtoto huyu ni mpole siyo mtundu na huko alikokuwa kwa mamake pengine baba aliona amchukue baada ya kuona mamake hajatulia na kadhalika.

Lakini pia inawezekana mama huyu aliyeletewa mtoto wa nje amegundua kuwa anazo tabia ambazo siyo nzuri, badala ya kumsaidia ili aendane na maadili mema anamnyanyasa. Watoto wengine huogopa kusema kwa kutishiwa na walezi wao.

Wako baadhi ya kinababa pindi wanapoleta watoto wa nje ya ndoa, na kuelezwa tabia zao mbaya hawakubaliani nalo. Huhisi kuwa mama mlezi hampendi ndio maana anamzushia mambo arudishwe alikokuwa.

Wako kinamama waliojikuta katika mazingira magumu pale wanaponyanyasa mtoto aliyeletwa kutoka nje ya ndoa. Nakumbuka kisa cha mama mmoja rafiki yangu aliyeletewa mtoto wa nje wa kiume miaka 9 ambaye alikuwa ameshindikana huko kwa mamake ili aje amlee.

Mumewe alikuwa kila akiondoka asubuhi hurejea saa tano za usiku hivyo tabia ya mwanae. Mama huyu yeye alikuwa na mtoto mmoja. Mtoto huyo wa nje akaanza tabia ya udokozi wa chakula au hata hela, uwongo. Kila alipojaribu kumwambia baba yake hakumwelewa.

Mwishoni baba akamwambia mkewe kwamba kama anataka amtoe huyo mtoto hapo nyumbani ni bora hata yeye (baba) aondoke. Anaponunua nguo anawabagua watoto.

Msomaji, iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilianzisha Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania. Sera hii Toleo la Pili la Machi 2008, ilainisha mambo mengi kuhusu ukatili dhidi ya mtoto.

Katika sura ya tano Hoja na Matamko ya Sera, kifungu cha 53 Hoja:ukatili dhidi ya watoto kinasema; Wapo watoto hapa nchini wanaofanyiwa vitendo viovu ambavyo ni pamoja na kutelekezwa, kutupwa, kupigwa, kuchomwa moto, kubakwa, kukeketwa, kutumiwa katika ukahaba, kuuzwa na kusafirishwa ndani na nje ya nchi.

Watoto wanaofanyiwa vitendo hivi huathirika kimwili, kiafya, kiakili, kisaikolojia na ukuaji wao. Sera inatamka kwamba serikali kwa kushirikiana na jamii na wadau wengine wa masuala ya watoto, iandae mikakati na program zinazolenga kuwalinda na kuwatunza watoto dhidi ya vitendo vya ukatili.

Pia serikali ielimishe wazazi na jamii kuwa jukumu la kuwalea watoto wao walio chini ya miaka minane ni lao na lisiachiwe watu wengine kama mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi na shule za bweni zilizo ndani na nje ya nchi.

Katika kifungu za 54 Hoja: Unyanyasaji na udhalilishaji wa watoto. Katika jamii zetu watoto wanafanyiwa vitendo vya ukatili visivyostahili kwa umri wao. Hali hiyo inawaathiri watoto kiafya na kisaikolojia badala ya kuwajengea uwezo kimaadili kwa maendeleo kama taifa tarajiwa la baadaye.

**Bila shaka vifungu vya sera hapo juu vimejibu utaratibu wa malezi ya mtoto wa Kitanzania. Je, una maoni au kisa cha maisha? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Walanguzi wa siasa kazini, uchaguzi na taswira 2025

TANGU kurejeshwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mfumo wa utawala, kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya Mtaa, Kijiji na Kitongoji, umekuwa ukifanyika katika kila kipindi cha miaka mitano.

Hivyo, kuanzia Juni Mosi, mwaka huu, wenyeviti wote wa vijiji, vitongoji na mitaa nchini, watarejesha mihuri ya serikali. Kurejesha kwao mihuri hiyo, ni ishara ya kumaliza muda wao wa kuhudumu katika wadhifa huo.

Tunakwenda katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, unaochukuliwa kama kipimo cha kutoa taswira ya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, utakaofuata mwaka 2025.

Bila shaka, wananchi wanakwenda kuchagua viongozi watakaowatumikia lakini ni lazima tuonye watakaokosa nafasi, wasiwe chanzo cha kuunda makundi.

Unapokosa, usianze kutengeneza makundi ili kukibomoa chama chako tukaanza kupambana maendeleo yasipatikane, tukaanza chuki, hapana huko tusifike.

Tuchagulieni kiongozi na mwanasiasa makini. Atakayetumia umakini wake kuteka fursa za kisiasa. Tunataka huyo kiongozi ajaye, kila anachokitafakari, anachokiandika, achokifanya na anachokitamka, kisilenge kutafuta na kupata fursa binafsi, kwa wakati huo au baadaye.

Hatumtaki mgombea ambaye ni msaka fursa au msaka tonge mtu mwenye ndimi nyingi ama sura nyingi.

Siyo mtuletee mgombea ambaye lengo lake ni kutaka anachokitaka. Kama kusema au kufanya lolote kunampa fursa, basi kada huyo atatenda. Hata chama anachokiongoza ni cha kusaka fursa. Ni kundi maarufu kama 'opportunists' (watu wanaosaka fursa au wanatafuta uongozi kwa ajili ya manufaa fulani).

Leo yako, kesho yako, ilenge kujielekeza kufanya mambo yanayoacha alama, na si kutafuta kiki ambazo mwisho wa siku hukumbukwi na wala hutoaminika tena.

Wako wagombea, ukiwaona au kuwafuatilia nyendo zao, utabaini anachokitafuta ni zaidi ya kufuja mali za umma na kujitafutia utajiri.

Mtu wa aina hii hafai kwa sababu amekaa kimaslahi zaidi. Nyie wanasiasa mnaotaka kugombea, jifunzeni namna bora ya kujenga hoja, namna bora ya kuonyesha kutokubaliana, kukubaliana na namna ya kushinda.

Kwa sababu amejiweka kwenye kundi la watu wanaotafrisiwa na jamii kama wasaka tonge. Si dhambi kutafuta fursa, ila hoja ni kwamba utaitendeaje haki fursa hiyo utakapoitapata!

Wanasiasa wengi wa aina hii, dhamira yao, sura yao na mwonekano wao unaonyesha dhahiri shahiri kwamba, ni watu wa kutaka wanachokitaka. Hataki kuona ukosoaji dhidi yake, hata kama kuna mantiki katika hoja fulani.

Ili uwe kiongozi mzuri na mtu anayeweza kupigiwa mfano na vijana wengine, jifunze kusikiliza wengine wanasema nini, jaribu kuwa mwenye huruma na mtu anayefanya rejea ya watu wengine walichokisema.

Ni jambo gumu lakini ni lazima tujitofautishe na wale walioharibu huko nyuma, taswira nzuri ya wanasiasa vijana, ambao waliaminiwa na kupewa nafasi nyeti za kuutumikia umma.

Labda kazi kubwa iko kwenye kujitofautisha na kujiweka kando na suala la mgongano wa maslahi.

Kufanikiwa kwako kutatokana na kuacha kudharau kufanyia kazi mlichokubaliana na walio juu yako au chini yako.

Kwanza, jenga uhalali wako, waaminishe unaotaka kuwaongoza ili waelewe na kuamini kile unachokisema.

Jenga uhalali wako, kwa kuwaondolea shaka ya mgongano wa maslahi na kile unachokisema.

Kwamba kwa nafasi uliyopewa uking'atuka au kutenguliwa uteuzi, utakuwa umeacha alama gani ya kukumbukwa.

Mwalimu wangu mmoja katika Somo la falsafa ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi pale Chuo Kikuu cha Iringa (UoI), aliniambia wakati fulani kwamba ukitaka kumjua mwanasiasa anakipenda chama au hakipendi mfanyie yafuatayo;-

Kwanza, mnyime madaraka anayoyataka, mnyang'anye haki yake ya kupata madaraka kwa njia ya kugombea halafu mkoseshe madaraka. Hapo sura nyingi alizonazo utaziona pasina shaka.

Ukitaka kumjua zaidi, mpime imani ya itikadi aliyo nayo, endesha mchakato unaonyima madaraka kwa makusudi. Utaona alivyo na ndimi nyingi.

Inahitajika nguvu kuwasukuma wengine kuupenda ushawishi wako, kuukubali na kubadilika.

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com. Simu ya mkononi: +255 715 545 490**







Familia ya Hume ilikuwa na kila aina ya furaha baada ya kumfanyia sherehe ya kumuaga binti yao Neema Japhet Hume ili kwenda kuanza maisha mapya ya ndoa. Hafla hiyo ilifanyika Novemba 26, mwaka jana katika ukumbi wa Lavender Hall Jijini Dodoma.



# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## NI AIBU KUVAA KIGODORO?

UNAPOPITA barabarani au kwenda katika sherehe mbalimbali za kijamii, ni jambo la kawaida kuwakuta idadi kubwa ya wanawake wakiwa na makalio au mapaja yaliyojaa vyema.

Wengi wao hawana maumbo yanayoonekana kwa nje, badala yake wameongeza vitu maalumu kwa ajili ya kunogesha umbo lake.

Vitu ambavyo vinatumika kuongeza makalio ni sponji iliyotengenezwa mfano wa kiungo husika na wengi huita 'kigodoro'.

Vazi hili la kigodoro hutumika na baadhi ya wanawake ili kuongeza shepu zao hasa sehemu za makalio na mapaja kwa matarajio ya kuwa na mwonekano mzuri zaidi.

Hata hivyo, wadau wa mitindo, wanatofautiana kuhusu umuhimu wa kuvaa vigodoro kwa wanawake.

Baadhi wanaunga mkono kwa kueleza kwamba limekuja kuziba ombwe linalowatesa baadhi ya wanawake ambao wanajiona hawajakamilika kutokana na kuwa na maumbile ya kawaida.

Wanasema vazi la kigodoro limesaidia kudumisha uhusiano wa watu ndani ya nyumba, hasa kutokana na wanaume wengi kupenda wanawake wenye maumbo yaliyokatika vyema.

Kwa kawaida wanaume hupenda wanawake wazuri, ndipo vazi la kigodoro linapotumika kujenga umbo bandia kwa ajili ya kukidhi kiu ya matamanio.

Kwa wale ambao wanaunga mkono matumizi ya vigodoro,wanaona ni vazi la kawaida na halishtui kama mtu anataka kuonekana vizuri.

Kwa upande wanaopinga matumizi ya vigodoro, wanaeleza kwamba ni udanganyifu kwani unaweza kuwaona wanawake kwenye sherehe wakiwa na maumbo mazuri, kumbe sivyo kwani baadhi wamefoji maumbo.

Wanaeleza matumizi yake yana uraibu na kumfanya mtumiaji kupatwa na ugonjwa ambao humfanya ashindwe kujikubali na badala yake anatumia vigodoro kujiumba kama anavyotaka mwenyewe.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# Tumia mvuke kubandua kope

UBANDIKAJI wa kope ni urembo unaopendwa na baadhi ya wanawake kupamba macho, lakini una changamoto nyingi wakati wa kuziondoa.

Ingawa kutafuta msaada wa mtaalamu wa urembo ni chaguo salama na la kuaminika, kuna njia kadhaa za kuondoa kope bandia ukiwa nyumbani.

Kupitia safu hii tutaelekezana njia rahisi za kukusaidia kuondoa kope ukiwa nyumbani kwako.

**Kutumia mvuke**

'Steam' au mvuke ni njia nzuri inayosaidia kulainisha gundi ya kope na kufanya upanuzi wa kope na hivyo kuwa rahisi kuondoa.

Zifuatazo ni hatua za kuzichukua kuondoa kope kwa kutumia mvuke:

Chemsha sufuria ya maji ya moto na uimimine kwenye bakuli kubwa.

Weka uso wako karibu na bakuli na funika kichwa chako na kitambaa ili kuzuia mvuke kutoka.

Ruhusu mvuke kuondoa kope taratibu kwenye macho kwa muda wa dakika 5-10 ili kupunguza gundi.

Futa taratibu kope na kitambaa laini au pamba ili ziweze kubanduka taratibu.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mtindi, matunda lishe bora ya watoto

MAZIWA ni chakula muhimu kwa ukuaji wa mifupa na kutoa madini muhimu katika lishe kwa watoto.

Maziwa ya mtindi ukichanganya na matunda ni chakula kizuri kwa mtoto asiyependa kula.

Mahitaji

Maziwa mtindi glasi moja, matunda safi yaliyokatwa katwa vipande vidogo mfano embe.

Namna ya kuandaa

Pima glasi moja ya maziwa na weka kwenye bakuli safi na kisha weka na vipande vya matunda unavyopendelea.

Changanya vizuri mchanganyiko wako na tayari kwa ajili ya kuanza kumlisha mtoto wako na atafurahia mlo huu.

Unaweza kumpa mlo huu saa nne mara baada ya kunywa uji asubuhi na utaona mabadiliko ya kuongezeka kwa uzito wa mwili wake.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# MSIMU WA KUPANGA NYUMBA UMEWADIA, USIKURUPUKE

## Ukale, usasa na rangi zilizotamba 2023



**Na Restuta James**

MWAKA 2014 umeanza kwa kishindo lakini ni muhimu tukijikumbusha mambo mazuri ya usanifu wa mapambo ya nyumba yaliyotamba mwaka jana.

2023 umefanikiwa kutoka kwenye zama za rangi ya kijivu iliyotamba miaka ya karibuni na kuongeza mchanganyiko wa bluu tulivu, nyeusi na dhahabu huku pia samani za ndani zikinogeshwa zaidi na uasilia uliochanganywa na ukisasa.

Mitindo 10 bora ya mapambo ya nyumbani kwa 2023 ni ubunifu wa kutumia vitu vya asili kama shanga, ukili, vibuyu, mbao, maboga na mitindo ya zamani kuboresha mandhari ya nyumba au migahawa.

Wataalamu wa mapambo wanaoutazama mwaka 2023 kama mwanzo wa ubunifu utakaodumu kwa miaka kadhaa kwenye eneo hilo kutokana na ubunifu wa mpangilio wa rangi, samani na bustani

Erica Mika, ambaye ni fundi rangi, anasema mwaka 2023 umekuwa wa mabadiliko makubwa katika mitindo ya ubunifu wa nyumba kuanzia ramani hadi mpangilio wa samani ambao utadumu kwa miaka kadhaa ijayo.

"Mitindo bora ya upambaji wa nyumba ya 2023 imetengeneza mazingira ya kufurahisha ya asili, na kuleta mambo mapya na ya zamani kwenye mchanganyiko. Kuongeza vipengele vya asili vyenye mguso wa kisasa na matumizi ya rangi ya dhahabu na nyeusi, kumeboreeha sana makazi," anasema.

Kwa mujibu wa Erica, rangi ya kijivu ni kama iko 'ukingoni' kwani kumekuwepo na mchanganyiko wa rangi kama 'gardenia' smoke, dhahabu na nyeusi zinazoendelea kufanya vizuri kwenye nyumba.

"Tunaona kwamba matumizi ya rangi ndio mfalme wa kubadili mandhari kwa mwaka huu. Tumeona namna ambavyo makochi, mito na picha za ukutani zinavyopaswa kuendana bila kusahau matumizi ya mbao yatakavyoendelea kutamba kwa muda mrefu," anasema Erica.

Hata hivyo, anasema rangi nyeusi na dhahabu, zitabamba zaidi mwaka ujao hasa katika eneo la jikoni na kuongeza kuwa nyeupe ni rangi isiyoepukika na pia ukale na ukisasa, kwenye samani hadi taa za umeme.

MSIMU wa kutafuta nyumba za kuishi umewadia, hivyo ni vema katika kipindi hiki kuwa makini zaidi katika kutafuta nyumba ambayo haitakuletea shida. Kwa maneno mengine hakikisha 'haukurupuki'.

Hakikisha unazingatia mambo muhimu kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa kupanga nyumba kwa ajili ya kuishi.

Moja ya mambo ya kuangalia ni mahali nyumba ilipo na umbali. Kumbuka kuna uwezekano mkubwa ukaona nyumba nzuri kwa mwonekano na ukatamani upange kwa ajili ya kuishi, lakini ikawa mbali zaidi au ikakulazimu kutumia pesa zaidi kwa upande wa usafiri.

Endapo unatumia usafiri wa umma, itakulazimu kila ukifika kituoni lazima utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo. Kwa hiyo ni lazima ufikirie kwa makini kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo, la sivyo unaweza ukashindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumba ni kuangalia kama nyumba hiyo itahitaji marekebisho makubwa.

Kuna baadhi ya nyumba huwa zinaonekana vizuri kwa nje lakini ndani zinahitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa ambazo hukutegemea. Kwa hiyo inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe.

Lingine ni masharti yanayokuwa yamewekwa kwenye nyumba husika. Baadhi ya wenye nyumba huweka masharti magumu na wakati mwingine mpangaji anapofika kuhitaji nyumba. Hawasemi ukweli lakini baada ya kulipia na kuanza kuishi ndipo huanza kuyasema kidogo kidogo kwa wapangaji. Kwa hiyo ni vyema kudodosa hilo kabla ya kufikia uamuzi wowote.


Hakikisha unausoma kwa makini mkataba kabla ya kulipia pesa yako kwenye nyumba. Wengi hufikiri ukishalipa kodi basi hakuna jambo la kwenda vibaya lakini mambo yanaweza kubadilika.

Kama ambavyo unakubali kwa kuandika kwamba utalipa kodi kwa wakati na kuitunza vyema, hakikisha pia na mkataba wako unausoma vizuri na kama kuna mambo ambayo mwenye nyumba anapaswa kuyatekeleza anafanya hivo, kama ilivyo kwako na kama ukibaini kama kuna kitu kinakufunga ni bora uulize mapema kabla ya kuingia rasmi kwenye nyumba.

Pia huu ni msimu wa mvua, hivyo hakikisha unazingatia endapo eneo la nyumba iliyopo hapajai maji, kwa sababu hilo nalo ni tatizo lingine linaloweza kukuletea shida.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
SIKU INGINE HILI BICHWA LAKO LIWE LINAFIKIRIA KUWA MIMI NI MKEO NASTAHILI KUTOLEWA 'OUT'
TUOMBE MUNGU
MIMI NIPELEKE POPOTE LAKINI HIYO NAULI SITOI
KAA NA HELA YAKO KANUNUE DONA ULE
NAULI ZIMEPANDA KOTEKOTE ACHA UTATA BHANA! AU ULIPIWE?
UNAHAMU YA MAKONDE YA KUKUFUNGULIA MWAKA
LIMEMSHUKA ALIDHANI ATASAPOTIWA LIANGALIE BICHWA LAKE!
MSIMU HUU MAFUNDI WENZAKO WOTE WAPO BIZA NA NGUO ZA 'MADENTI' KASORO WEWE!
KAZI NA GUBU ULIONA WAPI MTU ANATOBOA!
SASA TUOANE KUCHEZEWA SASA BASI
UMEMPATA KUNGWI AU SOMO NIKAMPE MAUA YAKE?
NIMEHAMA SASA KAA NA NYUMBA YAKO UNENEPE KA'PEPEKALE
WEWE SIMAMA NA MIZIGO YAKO KAMA UPO KWENYE FOLENI YA 'KIAMA' UKONDEANE MIGUU
KILA WANALOTABIRI KUHUSU MVUA INAKUWA KWELI, HIVI HAWA NIKIWAFATA SILIAZI KABISA HAWAWEZI KUNITABIRIA NDOA YANGU?
TANDALE 'GESTI'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
ALIYE JUU USIMNGOJE CHINI ATAKUCHELEWESHA...

# Wabunge 80 wafutiwa matokeo na tume ya uchaguzi DR-Congo

**Kinshasa,** DRC

TUME huru ya uchaguzi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (CENI) imefutilia mbali uchaguzi uliofanyika katika majimbo kadhaa.

CENI, imesema kumepatikana ushahidi wa kutosha kwamba sheria za uchaguzi zilivunjwa katika majimbo hayo.

Wabunge wateule, takriban 80 wameathiriwa ambao waliwania katika majimbo ya Kwilu,Yokama, Ubangi,na Equateur. Taarifa ya hatua hiyo, ilichapishwa Ijumaa, huku CENI ikisema kwamba ripoti ya uchunguzi uliofanyika ilionyesha kwamba katika uchaguzi wa ubunge na udiwani baadhi ya wagombea viti hivyo, walishiriki udanganyifu.

Aidha, tume hiyo ilisema kwamba uchaguzi uliofanywa na maofisa wa tume hiyo uliangazia kuvunjwa kwa sheria za kupiga kura na vile vile visa vya utovu wa usalama ambavyo vilishuhudiwa katika baadhi ya maeneo. "Jopo la uchunguzi la CENI linaendelea kupokea ripoti za uharibifu wa mali ya umma na vifaa vya kupigia kura, madai ya watu binafsi kupata vifaa vya kielektroniki vya kupigia kura, na vile vile kushambuliwa kwa wafanyakazi wa tume ya CENI," alisema Patricia Nyesa, Ofisa Mkuu wa CENI.

Tume hiyo ilisema pia inawachunguza wafanyakazi wao ambao wanadaiwa kushirikiana katika kuvunja sheria za uchaguzi za DRC. Huku CENI ikiendeleza uchunguzi wake, hatima ya walioathirika sasa iko mikononi mwa vitengo vya usalama na idara ya mahakama, wanatarajiwa kufunguliwa mashtaka mbalimbali.

Hayo yakijiri, Mahakama ya Kikatiba nchini humo, inaendelea kusikiliza kesi ya kupinga uchaguzi huo wa DRC wa Desemba 20, mwaka jana, iliyowasilishwa na mgombea huru wa urais, Theodore Ngoy, aliyelalamikia hali ilivyokuwa kwenye uchaguzi huo.

Aidha inatarajiwa kusikilizwa kesi iliyowasilishwa na kanisa nchini humo, kupataufafanuzi wa kikatiba kuhusu kuongezwa kwa muda wa kupiga kura, utatolewa katika siku chache zijazo.

**BBC**



Rais wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (CENI) nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Denis Kadima. **PICHA: JEUNE AFRIQUE**

## Abiria 177 chupuchupu kupoteza maisha ndege yatua kwa dharura

**OREGON,** MAREKANI

NDEGE ya abiria ilipoteza kipande chake wakati ilipokuwa inapaa angani, jambo lililomlazimu rubani kutua kwa dharua katika uwanja wa ndege uliopo katika jimbo la Oregon, nchini Marekani.

Ndege hiyo aina ya Boeing 737 Max 9 inayomilikiwa na kampuni ya ndege ya Alaska, ilirejea jijini Portland, dakika 35 baada ya kupaa angani, kipande cha nje cha dirisha moja kilipodondoka.

Kampuni hiyo ya ndege ya Alaska imesema kwamba abiria 177 na wahudumu wote, walitua salama.

Aidha ilisema kwamba itasitisha kwa muda safari za ndege zote 65 za aina ya 737 Max 9 ili kufanya ukaguzi wa kina.

Mamlaka ya safari za ndege nchini Marekani FAA imethibitisha kwamba ndege hiyo ya shirika la ndege la Alaska, ilitua salama.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya ndege ya Alaska, Ben Minucucci alisema: "Kila ndege itarejelea usafiri baada ya kuchunguzwa wa kina na kufanyiwa ukaguzi wa kiufundi na kupita uchunguzi wa usalama."

Minucci, alipongeza juhudi za wafanyikazi sita waliokuwa kazini kwenye ndege hiyo.

# Israel: Eneo la Gaza si salama kwa wakati huu

**Gaza City,** GAZA

ISRAEL imeonya kuwa eneo la Gaza si salama wakati huu mapigano yakiendelea. Jeshi la Israel limetekeleza mashambulio kusini mwa Gaza mapema Jumamosi.

Mashambulizi yanakuja wakati Umoja wa Mataifa (UN), ukionya kuwa eneo la Gaza kwa sasa sio salama kwa raia wa Palestina, vita vikiingia mwezi wa tatu sasa.

Mapigano hayo yalianza Oktoba 7, mwaka huu, baada ya wapiganaji wa Hamas kutekeleza shambulio kusini mwa Israel, hatua iliyosababisha Israel kujibu mashambulizi.

Makabiliano yakiendelea, matumaini ya kumalizika kwa vita hiyo yanaonekana kupungua, kutokana na misimamo ya kila upande.

Vita hivyo vimewaathiri pakubwa raia wa Gaza ambao wamepoteza makazi yao katika mashambulio kadhaa, mzozo wa kibinadamu ukiripotiwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa katika Ukanda huo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, anazuru nchini Uturuki, anatarajiwa kujadili suala la Gaza na Rais Recep Tayyip Erdogan.

Blinken pia atazuru mataifa kadhaa ya kiarabu kabla ya kuelekea nchini Israel na Ukingo wa Magharibi wiki ijayo.

Hivi karibuni, Israel imesema miongoni mwa mipango inayowekwa ni kuhakikisha kuwa, Gaza inaongozwa kwa kiwango kidogo na Wapalestina.

Kuhusu usalama, ukanda wote wa Gaza utakuwa chini ya Jeshi la Israeli, na kundi la Hamas halitaruhusiwa kuwapo.

Mapendekezo haya yanakuja, wakati huu jeshi la Israeli likiendeleza mashambulio ambayo kwa saa 24 zilizopita, mauaji ya watu yameendelea kushuhudiwa.

Wizara ya Afya kwenye ukanda wa Gaza inasema, vita hiyo imesababisha vifo vya zaidi ya watu 22,000 mpaka sasa.

Wakati huo huo, maofisa wa DRC kutoka upande wa Kinshasa na Congo-Brazzaville, wamekanusha ripoti kwamba wakimbizi wa Kipalestina watapewa makazi mapya Afrika ya Kati, kama sehemu ya makubaliano na Israel.

Gazeti la The Times of Israel mapema wiki hii liliripoti kwamba, Serikali ya Muungano ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, ilikuwa katika mazungumzo ya siri na Jamhuri ya Congo, ili kuwapa makazi maelfu ya watu kutoka Gaza. Ilinukuu chanzo katika baraza la mawaziri la usalama ambaye inasemekana alisema Congo ilikuwa tayari kuwapokea wahamiaji.

Msemaji wa Serikali ya Jamhuri ya Congo na Waziri wa Mawasiliano na Vyombo vya Habari, Thierry Moungalla alisema katika taarifa yake kwenye mtandao wa kijamii wa X kwamba nchi hiyo haijafanya mazungumzo na Israel kuhusu kuwapokea wahamiaji kutoka Gaza.

**RFI/BBC**

SAFU

MAKALA

# ITAKUHUKUMU



Na Magabilo Masambu

NI kweli kwamba mitandao ya kijamii kama facebook, Twitter, youtube, whatsap na Instagram imerahisisha sana mawasiliano yetu. Leo, kwa kutumia mitandao hiyo, tunaweza kuwasiliana na mtu yeyote duniani. Tunaweza kutuma ujumbe (sms), picha ama video au kupiga simu na kufanya mazungumzo.

Nje ya mawasiliano, wako wanaoitumia mitandao hiyo kibiashara ama kuuza bidhaa zao moja kwa moja, kutangaza au kufanya mawasiliano na wafanyabiashara wengine duniani. Lakini pia inatumika kuonyesha uwezo na vipawa vyetu. Mfano, kama una kipawa cha uimbaji, uigizaji, uandishi, siasa na kila aina ya sanaa, unaweza kuwaonyesha watu uwezo wako kirahisi.

Kinachosikitisha ni kwamba pamoja na faida zote hizo, wako wanaoamua kwa hiari yao kutumia mitandao ya kijamii kinyume cha maadili yetu kama Watanzania, ama kwa kujua au kwa kutojua madhara yake ya leo na kesho yao. Wanatuma picha au video za utupu mitandaoni bila kujali kwamba wana ndugu, jamaa na marafiki watakaozitazama.

Jambo ambalo hatulijui ni kwamba maisha ya mwanadamu ni fumbo kubwa kwa sababu tunajua tulikotoka lakini hakuna yeyote miongoni mwetu anayejua tunakokwenda. Hakuna anayeijua kesho yake. Tunaweza kudhani kwamba tulipo tumefika kumbe Mungu anayo mipango mingine na sisi. Wako watu ambao wanajiona waimbaji, waigizaji, wachekeshaji, waandishi na kadhalika na wamejiridhisha kwamba maisha yao yatakuwa hayo.

Mipango ya Mungu ni mikubwa huwa anamwinua yeyote, unaweza kuwa mchekeshaji leo kama Steve Nyerere, kesho ukawa Rais wa nchi kama alivyo Rais wa Ukraine, Volodyymyr Zelensky. Unaweza kuwa mchezaji mzuri sana wa mpira leo kama Mbwana Samata, kesho ukawa Rais kama alivyokuwa George Weah wa Liberia. Unaweza kuwa mwanamitindo leo kama Hamisa Mobeto kesho ukawa Mkuu wa Wilaya kama Jokate Mwegelo. Unaweza kuwa mwanamziki leo kama Gigy Money kesho ukawa mbunge kama mwanaFA na baadaye waziri, wako wengi siwezi kutaja wote lakini itoshe kusema kwamba yeyote anaweza kuwa chochote.

Ninachotaka kusema ni kwamba, nafasi tulizo nazo leo tusione hatuwezi kuwa wengine kesho maana yake matukio tunayoyafanya tukiwa na nafasi hizi leo, tuyafanye tukiwa waangalifu kwamba kesho na keshokutwa tunaweza kuwa watu watu mashuhuri kwenye jamii mambo yetu ya leo. Kwa hiyo mambo ya leo yasitufanye tukahukumiwa kesho. Ni mjinga tu atakayehukumiwa kesho utetezi uwe kwamba, nilifanya hayo kwa sababu nilikuwa msanii au ilinilazimu kufanya hayo kwa wakati huo. Lazima tutambuwe kwamba mitandao ya kijamii inahifadhi taarifa zetu milele.

Leo unapiga picha au video za utupu unazituma mtandaoni, kesho unakuwa Rais au kiongozi mashuhuri, waungwana wanakukumbusha kwamba kuna kapicha kako hapa unakakumbuka? Unaanza kutumia vyombo vya dola kuwaumiza wanaokukumbusha kwa mambo ulioyafanya mwenyewe ukiwa na akili timamu. Nani atalaumiwa katika hilo kama si wewe mwenyewe?

Siku hizi kumekuwapo na matukio machafu zaidi hasa yakiwahusu watoto wa kike. Baadhi wanatoa utetezi kwamba picha hizo zinavujishwa na watu wao wa karibu wakiwa na malengo wanayoyajua wao lakini kwa nini urekodi picha za namna hiyo na kumtumia mtu mwingine? Unadhani kufanya hivyo atakupenda sana? Jambo usilolijua ni kwamba thamani ya mwili wako ni kubwa kuliko kitu chochote. Matukio ya namna hiyo yanaweza kugharimu maisha yako. Baadhi tumesikia wakijiua baada ya picha zao kuvuja.

Nakubali kwamba kwa sababu ya ukuaji wa teknolojia, inawezekana ukarekodiwa bila kuwa na taarifa lakini uzoefu inaonyesha walio wengi wamekuwa wakirekodi na kupiga picha wenyewe au kuwaamini watu wao wa karibu na kwamba watazitunza. Inapotokea kutokuelewana, wanaona silaha ya kukumaliza ni kuachia picha na video zako. Ni muhimu sana kujilinda kabla ya kulindwa na wengine. Linda utu wako lakini zaidi heshima yako ya leo na kesho.

Wako wanaotumia picha zao kuongeza watazamaniji kwenye mitandao yao ya kijamii na inawezekana inawapatia fedha. Kwa maoni yangu bado una uwezo wa kuongeza watazamaji kwa kulinda maadii, utamaduni na utu wako kwa sababu si watazamaji wote wanafurahia kuona picha za utupu. Fedha zinazopatikana kwa njia hiyo hazitakuwa tofauti na za ukahaba au uuzaji wa bangi.

Jambo ambalo wengi pia hawajalifahamu ni kwamba, leo hii watu wengi wanakosa kazi duniani kwa sababu tu wamekuwa watumiaji wabaya wa mitandao ya kijamii. Unakwenda kuomba kazi kwenye kampuni fulani una vigezo vyote vya kielimu lakini wanaotaka kukupatia kazi wanaona wajiridhishe kwa kulitafuta jina lako kwenye mitandao. Kwa kufanya hivyo, wanakuta mambo ya ovyo, hivyo wanaona wakikupatia kazi unaweza kuharibu jina na taswira ya kampuni yao, hivyo wanaamua kutokukuchukua pamoja na kwamba unazo sifa za msingi.

Ushauri wangu kwa watumiaji wenzangu wa mitandao ya kijamii, ni muhimu matumizi yetu ya leo yalinde heshima yetu ya kesho. Tunaweza kuwa na watoto wadogo leo kesho watakuwa watu wazima na tutawapa tabu watakapokuwa na wenzao au wenyewe kuzitazama picha na video zetu.

Ishi leo kwa matarajio ya kuwapo kesho. Kazi yako leo isiuwe matumaini ya kuwa mtu mwingine kesho kwa kuwa lolote linawezekana. Ni jambo la muda tu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mume kakupa talaka, nduguzo wamekukataa utaishi wapi bibi?*



Na Adam Fungamwango

> **Wako waliofanya hivyo ikawa salama yao, hawakubahatika kugundulika. Lakini kuna ambao imekuwa bahati mbaya kwao mambo yakaharibika, habari zikavuja, zikamfikia mwenyewe, akaweka mitego yake, akamfuma mkewe, au kupata ushahidi wa usaliti na hapo ndoa inakuwa imekufa kifo cha asili.**

DUNIA hii ina mambo mengi sana na yanajirudia kizazi hata kizazi. Kuna wanaojifunza kupitia matatizo kizazi cha nyuma lakini wengine ni mpaka yawakute tena.

Leo tunawazungumzia baadhi ya kinadada na kinamama ambao pamoja na kuolewa wanakuwa na mambo ya kurukaruka. Kuna wanawake wanaodanganyika kirahisi sana na wanaume wa nje wakati wapo kwenye ndoa. Wanadanganyika na vitu vidogo vidogo ambavyo wao wanaona ni kama hawatimiziwi na waume zao.

Dada au mwanamama anaweza kupewa Sh. 10,000 na mumewe ya kununulia kijora, akafika dukani na kukuta bei yake ni Sh. 12,000.

Akatokea mwanamume yeyote hapo akaamua kumwongeza kiasi kilichopelea, huyo ataonekana wa maana sana kuliko mumewe. Mwanamume huyo anaweza kumdanganya na kuisaliti ndoa yake.

Baadhi ya wanawake hawathamini waume zao ambao wanawatunza kwa malazi, mavazi, kuwauguza wanapougua na kuwa karibu na familia zao zinapopata matatizo mbalimbali ya kijamii.

Katika yote hayo, mwanamume hutumia gharama na muda lakini yote kwa baadhi ya wanawake ni bure. Atakwenda kuisaliti ndoa yake kwa mwanaume ambaye atampa pesa nyingi kwa mara moja na haonekani tena.

Hamjui kwa shida zingine zozote zitakazomkabili. Hizo zitakuwa za mumewe tu.

Hiyo ni mifano tu ambayo imeshatokea sana, siyo kwenye kizazi hizi, bali tangu enzi na enzi.

Wako waliofanya hivyo ikawa salama yao, hawakubahatika kugundulika. Lakini kuna ambao imekuwa bahati mbaya kwao mambo yakaharibika, habari zikavuja, zikamfikia mwenyewe, akaweka mitego yake, akamfuma mkewe, au kupata ushahidi wa usaliti na hapo ndoa inakuwa imekufa kifo cha asili.

Ndoa nyingi zimevunjika kwa mtindo huo. Hata wanaoingia kwenye taasisi ya ndoa, wake kwa waume huwa wanatahadharishwa kuhusu mambo hayo kwa sababu yameshawatokea watu enzi na enzi, na yataendelea kwa sababu wapo ambao huwa wanajifunza kutokana na makosa ya watu wa kizazi kilichopita, lakini wengine ni mpaka yawakute.

Ukitaka kujua kuwa mambo haya yameanza zamani sana, katikati ya miaka ya 1970, mwanamuziki Marijani Rajabu akiwa na bendi ya Safari Trippers, aliachia kibao kiitwacho 'Hanifa', akimzungumzia mwanadada huyo aliyekuwa ndani ya ndoa lakini akafanya mambo yasiyoeleweka, mumewe akajua, akaachwa, ndugu wakamtenga, akabaki anatangatanga.

Ukiyasoma mashairi ya wimbo huu pamoja na kupangiliwa vizuri kisanii, ni kisa kinachotoa mafunzo kwenye jamii. Wimbo unaanza hivi:-

"Hanifa maisha yanakushinda, tazama unavyoishi sasa, nakupasha ujue wanawake wenzio sote twakucheka sana mama. Jinsi ulivyoishi na mumeo, Hanifa kwa maisha ya raha, chakula kwa fujo mavazi kila namna hata wenzi hatuna mama.

Wema aliyofanyaga hivyo, Hanifa ukamkorofisha, kwa kufuata mabwana kumbe walikudanganya sasa unatangatanga mama."

Hanifa alikuwa anatunzwa, anapendwa na kupata kila kitu kwa mumewe, lakini akapata mabwana waliondanganya. Wimbo unaendelea.

"Hivi sasa unajirudisha kwa bwana, na mume naye sasa hakutaki tena, sasa nambie mama utaishi vipi eee. Baba na mama yako pamoja na wandugu, baba na mama yako pamoja na wandugu, pia na wao hawakuthamini tena mama eee, pia na wao hawakuthamini tena Hanifa.

"Oooh bwana huna, hakutaki tena ee, oooh bwana huna, hakutaki tena ee, baba na mama, na mume Hanifa hunaaa. Baba na mama yako pamoja na wandugu, baba na mama yako pamoja na wandugu, pia na wao haku, pia nao hawakuthamini tena mama eee, pia na wao hawakuthamini tena Hanifa.

"Tena wanaona haya, tena hawana la kufanya, tena wanaona haya, tena hawana la kufanya Hanifa ni makosa yako mume wako hana makosa.

Lala lilo lololo, lala lilo hoo mama, baba na mama, na mume mwanangu hunaaa

Baba na mama yako pamoja na wandugu, baba na mama yako pamoja na wandugu, pia na wao haku, pia nao hawakuthamini tena mama eee, pia na wao hawakuthamini tena Hanifa."

Huu wimbo jinsi unavyoimbwa, unaonyesha wanaompasha ni shoga zake. Hanifa si mume tu, hata ndugu wamemtenga. Wanaona ndugu yao alikuwa kwenye ndoa yake akipata kila alichokuwa anataka. Hata wao pia waliambulia kutoka kwa shemeji na mkwe wao.

Atake nini tena mtoto wao. Sasa hivi mabwana wote wamemkimbia, anatangatanga. Hana pa kuishi, leo hapa kesho kule.

Baadhi ya wanawake watambue tu kuwa wanaume wengi huwapenda kwa sababu wako kwenye ndoa kwa sababu ya mteremko. Yaani hawahudumii moja kwa moja. Husaka pesa kwanza, wakizipata ndipo wanatafutwa. Zikiisha hawawatafiti.

Wanapoachika wanaonekana kama ni mzigo, kwa sababu mwanamke atakuwa anataka huduma za kila siku kama yupo kwa mumewe. Hapo ndipo wanapowakimbia. Akili 'kumkichwa', ukizubaa utaachwa feri.

**Tuma meseji 0716 350534.**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

## Wifi Kichefuchefu-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MWANAMKE aliyemrudisha tena kuwa binadamu. Aliyemfanya kujua duniani kuna kupenda na kupendwa. Aliyemfanya aanze kukaa nyumbani kwa muda mrefu zaudi kuliko baa. Mwanamke aliyemfanya akili yake ianze kufahamu kuwa siyo kila mwanamke ni mbaya kama alivyokuwa anadhani baada ya matendo aliyofanyiwa na mchumba wake wa mwanzo, Siwatu.

Rasmi Sauda akahamia nyumbani kwa Kassim, pika na kupakua. Baada ya mwaka mmoja kupita ilikuja taarifa kuwa baba yake Sauda ni mgonjwa huko Kondoa, hivyo inabidi aende kumuana.

Halikuwa jambo gumu kwa Kassim, alimkatia tiketi, akamfungashia na vijizawadi vya mama, pesa ya akiba kwa lolote litakalotokea kama akichelewa, na akamsindikika mwenyewe hadi kwenye Kituo cha Mabasi ya Magufuli.

Wiki mbili zilipita. Kukaa peke yake kulimchosha Kassim. Tayari adha hiyo alishaondokana nayo. Alishazoea kukaa na mpenzi wake Sauda.

Mwezi mmoja alivyotimia, akaambiwa na mchumba wake Sauda kuwa hawezi kurudi tena huko.

“Wamenizuia.” Aliongea kwa sauti dhaifu kwenye simu.

“Nani kakuzuia?”

“Baba.”

“Kwa nini?”

“Kasema mpaka wewe uje huku.”

“Kwani kuna nini Sauda? Mbona hutaki kuniweka wazi?”

“Dada keshawaambia huku kuwa ni mwanaume. Na nakaa naye. Kwa hiyo hata huu ugonjwa wa baba haukuwa wa kweli. Nilivyokuja huku nimesemwa kweli. Nikaambia nakaa na mwanaume muda wote bila kumpeleka kujitambulisha nyumbani.”

Kwa hiyo wanatakaje?” “Wewe uje ujitambulishe kwao, wakufahamu, mengine watakuja kukwambia wao wenyewe.” Yalikuwa ni mazungumzo ya simu kati ya Kassim na mpenzi wake Sauda.


Ingekuwa ni yale tu mapenzi ya mwanzo, Kassim wala asingejisumbua kwenda. Kwa sasa Sauda alikuwa amejaa moyoni mwake.

Hakuweza kufanya chochote bila Sauda. Kwake alikuwa ndiyo kila kitu.

“Hakuna yeyote aliyeleta barua huko?” Ni swali alilouliza kesho yake.

“Sijui, lakini sidhani, ningekuwa nimeshaambiwa. Ila ndugu yangu kama unanihitaji ufanye haraka uje.”

“Wala haina tatizo, waambie mwanzoni mwa mwezi nakuja. Nasubiria mshahara wangu mwisho wa mwezi.”




**“Nasikia mwaka sasa unaishi na mwanangu. Sisi kama wazazi na wajomba zake haturidhiki. Tuliposikia tukaona kwanza ngoja binti yetu akae, akifikisha mwaka tutaona hapo yeye mwenyewe keshaona panamfaa, kwa hiyo tutengeneza mazingira ya kuolewa na siyo kukaa kama hawara.” Mzee Semmy alimwambia Kassim.**

“Nakushauri uje na mtu. Huyo mtu ndiyo awe kama mshenga. Uwe na barua kabisa. Unajua angalau ukitoa barua tunaweza hata tukajenga hoja wakaniachia.” Sauda akashauri.

“Ni kweli mpenzi wangu, umetoa wazo la busara sana. Na ndicho ninachokupendea mpenzi wangu.” Akajibu.

“Ahsante sana mpenzi, nakutegemea utakuja, hutoniangusha.”

Wiki moja baadaye, Kassim alitimba Kondoa. Akapokewa vizuri na kukirimiwa na wakwe zake watarajiwa.

Hakuambiwa chochote hadi kesho yake jioni ndipo baba mkwe alipomwita chini ya mwembe na kumweleza anachokihitaji.

“Nasikia mwaka sasa unaishi na mwanangu. Sisi kama wazazi na wajomba zake haturidhiki. Tuliposikia tukaona kwanza ngoja binti yetu akae, akifikisha mwaka tutaona hapo yeye mwenyewe keshaona panamfaa, kwa hiyo tutengeneza mazingira ya kuolewa na siyo kukaa kama hawara.” Mzee Semmy alimwambia Kassim.

“Ni kweli mzee, nimeambiwa na mwenzangu, na ndiyo maana nimekuja na rafiki yangu, tumekuja na barua kabisa kesho atakukabidhi na baadaye hapo tuko tayari kupokea maagizo mengine kutoka kwako.”

“Vizuri, basi mwite huyo rafiki yako anikabidhi hiyo barua, halafu mimi kesho nitawaita ndugu na jamaa kwa ajili ya kuisoma na kutoa majibu.”

Kassim ambaye aliienda na rafiki yake Jeje, yeye ndiye aliyetumika mshenga.

Aliporudi kwenye nyumba ambayo walipewa na mzee Semmy ambayo aliijenga kijijini hapo kwa ajili ya wageni, Jeje alikwenda moja kwa moja kwa mzee na kumkabidhi barua.

Kesho yake Kassim na Jeje waliamua kuondoka kwenda mjini kutembea kwa sababu walijua wazi siku hiyo kuna kikao cha kusomwa barua hivyo haitokuwa vizuri wao kukaa.

Waliporejea tayari ndugu walikuwa wameshakaa kikao na kutoa majibu.

Barua ilikubaliwa na mahari ikapangwa, lakini ikafafanuliwa kuwa inaweza kutolewa kwa awamu.

Pamoja na hayo mzee Semmy alipinga kabisa binti yake Sauda kurejea Dar es Salaam. Baada ya chakula cha usiku Kassim alimuomba mama mkwe wake waondoke na binti yake na angefanya haraka kuja kufunga ndoa.

Mke akamwambia mumewe, lakini mzee Semmy alipinga. Akamwita mkwewe mtarajiwa na kumpasha.

“Najua umeshazoea kukaa na mwenzio, unaona tabu kukaa peke yako, lakini najua nyinyi vijana. Nikiwaruhusu kuondoka hapa itafika tena mwakani, sitaki.

Cha kufanya wewe nenda mjini, kajipange, uje hapa uoe moja kwa moja. Hata kama ukifunga ndoa ya siku hiyo unamchukua kwenda naye Dar sawa tu.”

Maneno ya baba mkwe wake walimfanya kulowa. Jasho lilimtoka. Akaona hakuna tena uwezekano wa kunyanyua mguu wake na mwanamke aliyempenda.

Akaona kwa mara nyingine tena atarejea Dar na kuendelea kuishi peke yake mpaka siku ambayo hata yeye mwenyewe haijui.

Ni kama mzee Semmy alisoma mawazo ya mkwewe mtarajiwa.

“Unasikia kijana. Mimi nachotaka binti yangu awe salama, au na ulinzi madhubuti, siyo anakaa ukimchoka umfukuze na yeye aambulie patupu. Nataka pia hata mimi mwenyewe niwe nakuja kumtembelea mwanangu. Hivi mnavyoishi mimi siwezi kuja kwa binti yangu. Ni matusi. Najua maisha ni magumu, kwa hiyo wala usitake sijui ufanye sherehe sijui nini, hapana.

Wewe njoo hapa siku yoyote ile, mimi nitafanya kasherehe kadogo tu, uje na ndugu zako hata wawili au mmoja kama huyu wa leo, nakuozesha, unaondoka na mke hapa, halafu huko kwenu mtajua wenyewe kama mkikaa baadaye kukusanya pesa mfanye sherehe kubwa, hiyo kivyenu, lakini sisi hapa tunajua binti yetu ameolewa.” Mzee Semmy akapigilia nyundo.

Hakukuwa na Kiswahili tena kwa Kassim. Ilibidi atii amri ya mzee.

Yeye na rafiki yake Jeje, wakaondoka, wakisindikizwa na Sauda hadi kwenye stendi za mabasi, tayari kurejea Dar es Salaam.

Mwezi mmoja baadaye, Kassim alijiandaa. Akapeleka taarifa kuwa anakwenda kuoa.

Mzee Semmy hakuifanya harusi ya mbwembwe. Watu walikula maandazi na chai. Kassim alikwenda Kondoa mjomba wake pamoja na yule yule aliyekwenda naye awali, Jeje.

Haikuwa harusi iliyochukua muda mrefu sana kama safari iliyofanywa kutoka Dar es Salaam kwenda Kondoa. Baada ya kumalizika majira ya usiku, mzee Semmy akamwambia mkwewe kuwa sasa anaweza kumchukua Sauda kwa sababu ameshakuwa mkewe rasmi.

“Sasa mnaweza kuondoka hata usiku huu.” Akamwambia mkwewe ambaye alikuwa ameipanga safari ya kurudi Dar kesho yake.

Hatimaye Kassim na sauda walirejea Dar kuanza maisha mapya ya ndoa. Mwanzo walikuwa wanakaa tu kama mahawara.

Wakati Sauda wakidhani kuwa sasa anarejea Dar kuishi na umewe kwa raha mustarehe, kumbe anakwenda kulijua jiji.

INAENDELEA JUMAPILI

## HABARI BURUDANI

# OTILE BROWN APATA MENEJA MPYA

MWIMBAJI na mtunzi nyimbo kutoka nchini Kenya Otile Brown amemtambulisha meneja wake mpya baada ya kuachana na Noriega ambaye alikuwa akimsimamia kazi zake.

Otile Brown kupitia ukurasa wake wa Instagram, amewaambia mashabiki zake kwamba meneja wake mpya anayeitwa Mumbi Maina atakuwa nahodha sahihi katika safari yake ya kimuziki.

„Tunamkaribisha nahodha wetu mpya,tulifurahishwa na uongozi tunapoanza miradi ya kusisimua tukiwa pamoja. Hapa tumefika kutokana na ushirikiano, ukuaji na mafanikio mapya,@ ameandika.





# ROMA, CHID WATATA KWENYE 'NASIKIA HARUFU'

RAPA mwenye mashairi ya utata, Roma Mkatoliki, amemrudisha upya katika jukwaa la muziki, Chid Benzi, baada ya ngoma yao kuwa gumzo.

Ngoma hiyo mpya inayoitwa 'Nasikia Harufu' imetambulishwa siku chache zilizopita na imepata watazamaji wengi katika mtandao wa You Tube.

Katika wimbo huo, Chid Benzi na Roma Mkatoliki wameonekana kuonyesha uwezo wao wa kuchana na kusababisha wapenzi na mashabiki wa muziki ambao wameeleza ujio huo umemrudisha Chidi katika nafasi yake.

## ZISIKUPITE

### MAN KUMLIPA SANCHO
KLABU ya Manchester United italipa sehemu kubwa ya mishahara ya Jadon Sancho ikiwa winga huyo wa Uingereza mwenye umri wa miaka 23 atarejea Borussia Dortmund kwa mkopo. **(i Sport)**

### TOMORI ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal imeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa AC Milan na England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 26. **(Football Transfers)**

### JUVE YAJITOA KWA PHILLIPS
JUVENTUS imejiondoa kwenye mbio za kumsaka kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips, 28, ambaye pia anawaniwa na Newcastle United. **(Sun)**

### DIER ATAKIWA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich wanafanya mazungumzo na mlinzi wa Tottenham Hotspur na England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 29 kama moja ya chaguo la beki wa kati. **(Athletic)**

### WEST HAM KUMUUZA AGUERD
KLABU ya West Ham iko tayari kumuuza mlinzi wa Morocco, Nayef Aguerd mwenye umri wa miaka 27 mwezi huu, ikiwa kocha David Moyes atapata mbadala wake kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili. **(Standard)**

### ....ROME, MILAN ZAMTAKA
AS Roma na AC Milan zinataka kumsajili Nayef Aguerd, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa pauni milioni 30. **(CaughtOffside)**

### DRAGUSIN AWINDWA
KLABU ya Tottenham Hotspur itakabiliwa na ushindani kutoka kwa Napoli kumsajili beki wa Genoa raia wa Romania, Radu Dragusin mwenye umri wa miaka 21. **(ESPN)**

### MARTIAL ATAKIWA UTURUKI
FENERBAHCE ya Uturuki ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 28. **(Takvim)**

### BARCO NA BRIGHTON
KLABU ya Brighton wameanzisha kipengele cha kutoa pauni milioni 10 kwa mlinzi wa Boca Juniors na Argentina chini ya umri wa miaka 20, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 19, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Manchester City, Liverpool, Chelsea na Real Madrid. **(TyC Sports)**

### SUMMERVILLE AVUTIA
ASTON Villa na Brighton zinavutiwa na winga wa Leeds United Mholanzi Crysencio Summerville mwenye umri wa miaka 22. **(Football Insider)**

### MOURINHO AKANUSHA
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho amekanusha kuwasiliana na Shirikisho la Soka la Brazil (CBF) kwa nia ya kuwa kocha wa timu ya taifa mnamo Julai 2024. **(ESPN)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: 'NIMEMIS' KUCHEZA NA MESSI

Mfaransa huyo amesema kucheza na messi anakuwa na uhakika wa...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amesema amemisi kucheza pamoja na mchezaji mwenzake wa zamani, Lionel Messi.

Mshindi mara nane wa tuzo ya Ballon d'Or Messi alicheza misimu miwili na Mbappe katika klabu ya PSG kabla ya kujiunga na Inter Miami kama mchezaji huru Julai 2023.

Wakati wakiwa pamoja, Mbappe na Messi walishinda mataji mawili ya ligi na moja la Coupe de France ingawa Messi na mchezaji mwenza Neymar walizomewa katika miezi yao ya mwisho katika klabu hiyo baada ya kutolewa mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora.

„Mara zote utamisi kucheza na Leo Messi," alisema Mbappe akiiambia Amazon Prime Sport.

„Kwa fowadi kama mimi, unapenda kukimbia mbele, ukiwa naye katika timu yako una uhakika unaweza kupata mpira.

"Kwa ujumla, kucheza naye, imekuwa maalum. Messi anastahili heshima zote na kwa kweli nchini Ufaransa, hakupata heshima aliyostahili."

Mbappe, ambaye alifunga Jumatano na kuisaidia PSG kutwaa Kombe la Ufaransa, alisema baada ya mechi hiyo kuwa bado hajafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa analengwa kwa muda mrefu na Real Madrid na mkataba wake na PSG unamalizika msimu huu wa joto.

„Bado sijafanya uamuzi wangu," alisema Mbappe akiwaambia waandishi wa habari. „Sijafanya chaguo".

„Lakini kama nilivyosema, muhimu zaidi ni mataji. Tumeshinda moja tayari na tumedhamiria kushinda zaidi."

Mbappe mwenye umri wa miaka 25, alikuwa karibu kujiunga na Madrid msimu wa joto wa 2022 kabla ya kutangaza kubakia Parc des Princes.

Mbappé, ambaye alisajiliwa kutoka Monaco mwaka 2017 ndiye mfungaji bora wa muda wote wa PSG, ameshinda mataji matano ya Ligue 1 akiwa na klabu hiyo.

PSG wanaongoza Ligue 1 kwa pointi tano na watamenyana na Real Sociedad katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa.




# BRAZIL WAMTIMUA KOCHA WA MUDA

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

KOCHA wa muda wa Brazil, Fernando Diniz ametimuliwa na shirikisho la soka nchini humo (CBF).

CBF ilisema katika taarifa yake kwamba Rais Ednaldo Rodrigues alimweleza Diniz kwamba anataka „kuendeleza mchakato wa kuchagua kocha wa kudumu.“

Diniz aliajiriwa kama kocha wa muda wa mabingwa hao mara tano wa Kombe la Dunia Julai mwaka jana kwa mkataba wa mwaka mmoja, huku shirikisho hilo likiwa na uhakika wa kumteua kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti msimu huu wa joto baada ya kumalizika kwa mkataba wake na wababe hao wa Hispania.

Hata hivyo, Ancelotti alisaini mkataba mpya na Madrid hadi 2026.

Rodrigues sasa ameamua kuajiri mbadala wa kudumu wa Tite, ambaye alijiuzulu kufuatia kutolewa kwa Brazil katika robo fainali kwenye Kombe la Dunia la 2022.

„CBF inamshukuru Fernando Diniz kwa kazi yake, kujitolea kwake, umakini wake na kwa changamoto ya kuifufua Brazil,“ ilisema taarifa hiyo.

Uamuzi huo ulichukuliwa siku moja baada ya Rodrigues kurejea kwenye nafasi yake kufuatia uamuzi wa Mahakama ya juu zaidi ya Brazil.

Rodrigues na wasimamizi wake wote walikuwa wameondolewa kazini Desemba 7 baada ya mahakama ya Rio de Janeiro kutoa uamuzi kuhusu makosa katika mchakato wa uchaguzi wa 2022.

Kocha wa São Paulo, Dorival Junior ndiye anayeongoza kwa sasa kuchukua nafasi ya kocha mkuu wa kudumu, huku Rodrigues akiwa tayari amezungumza na rais wa São Paulo, Julio Casares, vyanzo viliiambia ESPN Brasil.

São Paulo hawataki kumuacha kocha wao aondoke bure na wameiomba CBF kulipa ada ya kusitisha mkataba wa Dorival, ambayo itakuwa karibu dola 920,000, vyanzo vilisema.

Wakati akiwa na Brazil, Diniz aliendelea kuwa kocha mkuu wa Fluminense, ambaye aliiongoza kutwaa taji la Copa Libertadores Novemba.

# Watano kung'olewa Man Utd

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imepanga kuchinja nyota wao watano kuanzia dirisha la usajili la Januari, 2024 na lile kubwa ili kupata fedha za kushusha majembe mengine.

Hii inakuja siku chache baada ya tajiri Sir Jim Ratcliffe kukamilisha ununuzi wa hisa zake kwa asilimia 25, na sasa yuko tayari kwa usimamizi na uendeshaji kikosini hapo.

Bilionea huyo wa Uingereza ana nia ya kubadilisha muundo wa usajili wa United na kuondokana na porojo za gharama kubwa zilizokuwa zikifanywa na utawala wa zamani.

Tayari United imewaruhusu Donny van de Beek kutua Eintracht Frankfurt kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huku, Sergio Reguilon akikatishiwa mkataba wake na kurejea Tottenham baada ya kudumu



kwa miaka minne Old Trafford.

Kocha wa Man United, Erik ten Hag anatazamiwa kuendelea kuwaruhusu nyota wengine zaidi kwenye usajili huu wa dirisha dogo.

Nyota walio njiani kuondoka kuanzia dirisha hili na lile kubwa ni Jadon Sancho ambaye anatarajia kwenda kwa mkopo Borussia Dortmund, Anthony Martial mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na Ten Hag hana mpango na Casemiro ambaye kiwango chake kimeshuka, sasa United wanasubiri ofa kubwa kutoka klabu za Saudi Arabia.

Raphael Varane ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu amegoma kuongeza tena naye ataondoka.

Sofyan Amrabat pia anatajwa kuwa atarudishwa Fiorentina baada ya kushindwa kuonyesha uwezo wake, akiwa United kwa mkopo.

# Waarabu warudi kwa Kevin de Bruyne

**RIYADH, Saudi Arabia**

WAARABU wa Saudi Arabia wameripotiwa kuanza tena mazungumzo na wakala wa kiungo wa Manchester City, Kevin de Bruyne ili kuipata saini ya kiungo huyo katika dirisha hili ama lijalo.

Waarabu hawa walijaribu kutaka kumsajili staa huyu katika dirisha lililopita lakini ilishindikana baada ya Man City kudaiwa kukataa kumuuza.

Hata hivyo, katika kipindi hiki, mabosi wa Man Ciy wameonyesha nia ya kutaka kumpiga bei kwa sababu amekuwa akipata majeraha ya mara kwa mara, ambayo yamesababisha awe nje ya uwanja kwa muda mrefu hususan kwa msimu huu.

De Bruyne staa wa kimataifa wa Ubelgiji ambaye mkataba wake Man City unatarajiwa kumalizika mwaka 2025, msimu huu amecheza mechi mbili tu na kutoa asisti moja hiyo yote ikichangiwa na majeraha aliyokuwa anauguza.

Fundi huyu anapokea mshahara wa Pauni 400,000 kwa juma na kwa mujibu wa taarifa huenda akienda Saudia atapokea mshahara mnono zaidi.

Inadaiwa mshahara mpya akikubali kwenda unaweza kuwa mara mbili ya anaopokea sasa Man City.



HABARI MICHEZO

# TAIFA STARS KUTESTI MITAMBO LEO MISRI

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ,Taifa Stars' leo inacheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Taifa ya Misri ikiwa ni mchezo wa kujipima na kutesti mitambo yake kuelekea kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) yatakayoanza Januari 13 nchini Ivory Coast.

Mpaka kufikia leo wachezaji wote wameripoti kambini ambapo jana kundi la mwisho likiwa na wachezaji nane walijiunga na wenzao kambini, wachezaji hao ni Tarryn Allarakhia, AbdulMalik Zakaria, Abdi Banda, Mohammed Omar, Novatus Miroshi, Morice Abraham na Miano Danilo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche alisema wachezaji wote wameripoti kambini na wako tayari kwa mchezo huo wa leo dhidi ya Misri wa kujipima kabla ya kwenda Ivory Coast kwa Fainali hizo.

Mchezo huo wa kirafiki unatarajiwa kuanza saa 12:00 jioni kwa saa za Misri ambap ni sawa na saa 1:00 jioni kwa saa hapa za Afrika Mashariki.

Amrouche alisema muunganiko wa wachezaji wote ni mzuri, utimamu wa mwili wa nyota uko vizuri na mechi yao ya leo itazidi kumpa mwanga wa kufahamu mapungufu ya kikosi chake na kuyafanyia kazi kabla ya kwenda kwenye fainali hizo za Afrika.

"Tunacheza mechi dhidi ya Misri kesho (leo), kama benchi la ufundi mchezo huu utatoa mwanga kwetu wa kuona sehemu gani ya kufanyia kazi mapema , pia kuendelea kutengeneza muunganiko mzuri na wachezaji waliopo hapa kambini," alisema Amrouche na kuongeza,

„Wachezaji walikuowepo kambini wanaendelea vizuri, kinachonifurahisha ni kuona uelewano mzuri wa timu yangu na tupo tayari kwa ajili ya mashindano," alisema kocha huyo.

Naye mmoja wa wachezaji waandamizi wa kikosi hicho, Mohammed Hussein ,Tshabalala' alisema kambi yaso nchini humo inaendelea vizuri na tayari kikosi chao kimekuwa na muunganiko mzuri wa wachezaji na wao kama wachezaji wapo tayari kupambana na ana imani mechi ya leo itazidi kuwapa uimara.

"Tuko tayari kwa mechi yetu ya kirafiki dhidi ya Misri itasaidia kumpa mwalimu mwanga wa kuona mapungufu ya kikosi chake, wapi afanyie kazi na kwenye ubora apaimarishe, tunaenda katika michezo ya ushindani, tunaenda katika uwanja wa mapambano, tutahakikisha tunafanya vizuri katika hatua ya makundi ya AFCON," alisema Hussein.

Stars iko kambini chini Misri ikijiandaa na Fainali hizo za AFCON ambapo wapo katika Kundi F pamoja na timuza Morocco, DR Congo na Zambia huku mchezo wao wa kwanza wakitarajiwa kucheza Januari 17 dhidi ya Morocco.



Wachezaji wa mpira wa Kikapu, wa timu ya vijana wanawake,wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA:JUMANNE JUMA**

# Wazawa wawazidi wageni magoli ya vichwa

**Na Adam Fungamwango**

WASHAMBULIAJI wazawa katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Habib Kyombo wa Singida Fountain Gate na Pius Buswita wa Namungo wanaongoza kwa mabao ya vichwa, kila mmoja akifunga mabao matatu na kuwazidi washambuliaji wote wa kigeni kwenye ligi hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, wachezaji hao wamefunga idadi hiyo ya mabao ambayo ni ya juu kwa wachezaji kufungaa kwa kichwa.

Wachezaji hao wa Kibongo wameonekana kuwapiga bao mastraika wengi wanaocheza soka la kulipwa kwa kusajiliwa na klabu mbalimbali nchini mpaka kufikia raundi ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ikumbukwe kuwa Kyombo alishawahi kuichezea Simba na Buswita ameshawahi kuichezea Yanga kwa nyakati tofauti.

Katika kile kinachoonyesha kuwa wachezaji wa Kitanzania wanaonekana wapo vizuri kwenye mabao ya vichwa, wanaoshika nafasi ya pili ni Feisal Salum wa Azam FC, Charles Semfuko wa Coastal Union ambao wote wamefunga mabao mawili ambapo katika orodha hiyoanaingia mchezaji wa kigenu, Kennedy Musonda wa Yanga.

Twakwimu hizo zinaonyesha mchezaji wa kigeni pekee aliyeingia kwenye orodha hiyo ni Musonda ambaye pia anaichezea timu ya taifa ya Zambia inayojiandaa na fainali za AFCON zitakazoanza Januari 13 nchini Ivory Coast.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha mashindano ya Mapinduzi Cup pamoja na fainali hizo za AFCON.

## Simba yashusha kiungo mkabaji

INATOKA UK. 24

„Maamuzi ya Charamba anayo Kocha Benchikha, jukumu letu sisi ilikuwa kumsafirisha kutoka Zimbabwe kumleta hapa Zanzibar na kumpa nafasi ya majaribio, lakini mwamuzi wa mwisho ni kocha wetu, amemuona kwa dakika 45, yeye ndiye atakayesema nini kifanyike„" alisema Ahmed.

Kuhusu mchezaji huyo kupewa jezi namba 24 na kuitumia kwenye mchezo dhidi ya APR huku jezi hiyo ikiwa ni ya Aubin Kramo aliyokabidhiwa tangu kuanza kwa msimu huu, Ahmed alisema ni Kramo mwenyewe ndiye aliyeikataa jezi hiyo.

„Kramo aliporejea tu kutoka kwenye majeraha aliomba abadilishiwe jezi, anataka jezi nyingine kwa hiyo moja kwa moja ikawa wazi, tukampa Charamba afanyie majaribio, lakini niwatoe hofu mashabiki na wanachama wa Simba juu ya Kramo, mchezaji huyu bado yupo sana Simba na ameshapona," alisema Meneja Habari huyo.

## Yanga SC yaionya APR kombe la Mapinduzi

INATOKA UK. 24

tunaweza kumtumia kwenye hatua ya nusu fainali au fainali kama tutafanikiwa kuingia," alisema N'Daw.

Akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, Denis Nkane amesema wamejiandaa vizuri ingawa wanajua ugumu wa mechi hiyo dhidi ya APR.

„Tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunakifanya kilichotuleta huku, michuano ya Kombe la Mapinduzi ni migumu msimu huu tangu ilipoanza, na hata mechi hii haitokuwa rahisi kwa sababu APR ni timu kubwa siyo Afrika Mashariki na Ukanda wa CECAFA tu, bali hata katika bara letu la Afrika, ina wachezaji wazoefu na ukizingatia hii ni hatua ya mtoano kwa timu zilizofuzu kutoka hatua ya makundi, hatutarajii mchezo mwepesi," alisema Nkane.

Zipo taarifa kuwa Yanga imeita baadhi ya wachezaji wake waliokuwa wamewapa mapumziko akiwemo Pacome Zouzoua, Salum Abobakar ,Sure Boy', Khalid Aucho, na wengineo kwa ajili ya mechi hiyo na zinazofuata.

Yanga imetinga hatua ya robo fainali baada ya kuliongoza Kundi C, ikiwa na pointi saba, huku APR ikitinga hatua hiyo kama ,best looser' wa Kundi B, ikishika nafasi ya tatu na pointi zake nne.

Robo fainali nyingine itapigwa kesho ambapo mchezo wa kwanza, Azam FC itaumana na Singida Fountain Gate saa 10 jioni wakati mchezo wa pili, Simba itaumana na Jamhuri saa 2:15 usiku.

Michezo
Jumapili Januari 7, 2024
Nipashe

Mbappe: 'Nimemis' kucheza na Messi UKURASA 21



# SIMBA YASHUSHA KIUNGO MKABAJI

**●●● Ni raia wa Senegal, asaini mkataba wa miaka miwili hatma ya Charamba mikononi mwa Benchikha, Kramo aungana na wenzake, akataa...**

**Adamu Fungamwango na Saada Akida**




WAKATI Kocha Abdelhak Benchikha akipewa rungu la kuamua kama mchezaji Michael Charamba raia wa Zimbwabwe ambaye yupo kwenye majaribio asajiliwe au waachane naye, Simba jana imetangaza rasmi kumsajili kiungo mkabaji wa kimataifa kutoka Senegal, Babacar Sarr mwenye umri wa miaka 26 kwa mkataba wa miaka miwili.

Kiungo huyo aliyeichezea US Monastir ya Tunisia msimu uliopita anakuwa mchezaji wa pili kutambulishwa na klabu hiyo kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo baada ya Saleh Karabaka aliyetambulishwa hivi karibuni akitokea JKU ya Zanzibar.

Sarr, akiwa na Monastir iliyocheza na Yanga kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika msimu uliopita, alicheza mechi iliyoikutanisha timu yake hiyo dhidi ya Al Nassr iliyokuwa na Cristiano Ronaldo ndani katika mechi za Klabu Bingwa kwa Nchi za Kiarabu.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Mfalme Fahd, Saudi Arabia, Julai 31 mwaka jana, US Monastir ilipokea kichapo cha mabao 4-1, Ronaldo akifunga bao moja kati ya hayo, Sarr akicheza dakika zote 90.

Awali, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema tayari mpaka sasa wameshafanya usajili wa wachezaji wanne, wawili wa kigeni na wawili wa Kitanzania, huku mmoja tayari wakiwa wameshamtangaza.

„Dirisha dogo la usajili linafungwa Januari 15, tumesajili wachezaji kama wanne kilichobaki kwa sasa ni kuwatangaza tu, kuna wachezaji wa ndani wawili muda si mrefu tutawatangaza, ni mashine hasa, Simba tukisajili mchezaji wa Kitanzania basi lazima awe wa hadhi ya juu nchini, halafu kuna vinu vya nyuklia, wachezaji wawili wa kigeni, tayari tumeshawasajili, kwa hiyo mpaka tutakapoondoka hapa Zanzibar tutakuwa tumefanya usajili kwa asilimia 98, sisemi kama hao tuliowasajili tumemaliza, hao ni wale ambao tayari tumemalizana nao," alisema.

Habari za ndani kutoka klabuni humo zinasema wachezaji wa Kitanzania waliotia wino na kwa sasa wanasubiri kutangazwa ni Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar na Edwin Barua kutoka Prisons.

Pia zipo tetesi kuwa kocha Benchika amevutiwa mno na uwezo wa beki Jean Engola, raia wa Cameroon anayeichezea JKU kwa sasa lakini alipita kwenye klabu ya La Galaxy II ya Marekani na kama mambo yataenda sawa huenda naye akavaa uzi mwekundu.

Ahmed pia amesema mchezaji Michael Charamba aliyecheza mechi ya juzi ya Kombe la Mapinduzi kwenye Uwanja wa New Amaan Complex dhidi ya APR ya Rwanda, hajasajiliwa kama ilivyoripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari bali alikuja kwenye majaribio.

INAENDELEA UK. 23

## Yanga SC yaionya APR kombe la Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Msenegal, Moussa N'Daw ameahidi kuingiza kikosi imara kwa ajili ya kuivaa APR ya Rwanda katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Mapinduzi huku akiwatahadharisha wapinzani wao watarajie kukutana na mchezo mgumu leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Mchezo huo ambao utakuwa robo fainali ya pili kwa leo ukitanguliwa na robo fainali ya kwanza kati ya Mlandege dhidi ya KVZ mchezo utakaochezwa saa 10 jioni kwenye uwanja huo wa Amaan.

N'Daw alisema baada ya kuchezesha wachezaji wengi wa kikosi cha pili, leo wataingiza kikosi kilichokamilika kwani wanataka kupata ushindi dhidi ya timu ngumu ya APR.

„Leo tutaingia kamili, katika baadhi ya mechi zilizopita tulikuwa tunachezesha wachezaji wa kikosi cha vijana chini ya miaka 20, lakini katika mechi hii tutabadilika kwa sababu tunakwenda kucheza na timu ya APR, ni timu nzuri, yenye wachezaji wazuri, imecheza mechi za awali za Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini sisi ni Yanga, nia yetu na dhamira yetu ni kushinda kila mechi," alisema kocha huyo.

Aidha, alisema wachezaji wote wapo tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wanachotaka ni kwenda hatua ya nusu fainali mpaka na baadae fainali ili kuweza kujiweka katika mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa wa mashindano hayo.

Kocha huyo alipoulizwa kuhusu mchezaji wao mpya Agustin Okrah kama atakuwepo kwenye mchezo wa leo, amethibitisha kuwa nyota huyo hawezi kucheza mchezo wa leo.

„Kwanza tunaangalia afya yake ndio kitu muhimu, Okra yupo vizuri baada ya kupata masaibu lakini hatuwezi kumtumia mchezo wa leo, tunampa muda wa kuzidi kuimarika,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042